**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2020 - 2025**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. | Zubeir Ali Maulid | - | SPIKA |
| 2. | Mhe. | Mgeni Hassan Juma | - | Naibu Spika/Nafasi za Wanawake |
| 3. | Mhe. | Mwanaasha Khamis Juma | - | Jimbo la Dimani |
| 4. | Mhe. | Shaaban Ali Othman | - | Jimbo la Mpendae |
| 5. | Mhe. | Hemed Suleiman Abdulla | - | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Uteuzi wa Rais |
| 6. | Mhe. | Mudrik Ramadhan Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji/ Jimbo la Bububu. |
| 7. | Mhe. | Masoud Ali Mohammed | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Ole. |
| 8. | Mhe. | Haroun Ali Suleiman | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora/Jimbo la Makunduchi. |
| 9. | Mhe. | Jamal Kassim Ali | - | MBM/Waziri wa Nchi, (OR) Fedha na Mipango/Jimbo la Magomeni. |
| 10. | Mhe. | Dkt Khalid Salum Mohamed | - | MBM/Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi/Jimbo la Donge. |
| 11. | Mhe. | Dkt. Soud Nahoda Hassan | - | MBM/Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo/Jimbo la Paje |
| 12. | Mhe. | Simai Mohammed Said | - | MBM/Waziri wa Elimu na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Mafunzo ya Amali/Jimbo la Tunguu |
| 13. Mhe. | Tabia Maulid Mwita | - | MBM/Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo/ Uteuzi wa Rais |
| 14. Mhe. | Riziki Pembe Juma | - | MBM/Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi/ Nafasi za Wanawake |
| 15. Mhe. | Rahma Kassim Ali | - | MBM/Waziri Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi/Nafasi za Wanawake |
| 16. Mhe. | Suleiman Masoud Makame | - | MBM/Waziri wa Maji, Nishati na Madini/Jimbo la Chonga |
| 17. Mhe. | Abdulla Hussein Kombo | - | MBM/Waziri wa Uchumi wa Bluuu na Uvuvi /Jimbo la Mkoani |
| 18. Mhe. | Lela Muhamed Mussa | - | MBM/Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale/Nafasi za Wanawake |
| 19. Mhe. | Abdalla Abasi Wadi | - | Jimbo la Nungwi |
| 20. Mhe. | Ali Abdulgulam Hussein | - | Jimbo la Jang'ombe |
| 21. Mhe. | Ali Suleiman Ameir | - | Jimbo la Pangawe |
| 22. Mhe. | Ameir Abdalla Ameir | - | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 23. Mhe. | Anna Athanas Paul | - | Uteuzi wa Rais |
| 24. Mhe. | Asha Abdalla Mussa | - | Jimbo la Mahonda |
| 25. Mhe. | Azza Januar Joseph | - | Nafasi za Wanawake |
| 26. Mhe. | Bahati Khamis Kombo | - | Jimbo la Chambani |
| 27. Mhe. | Bakar Hamad Bakar | - | Jimbo la Wawi |
| 28. Mhe. | Bihindi Hamad Khamis | - | Nafas iza Wanawake |
| 29. Mhe. | Fatma Ramadhan Mohamed (Mandoba) | | Nafasi za Wanawake |
| 30. Mhe. | Habibu Ali Muhamed | - | Jimbo la Mtambwe |
| 31. Mhe. | Haji Omar Kheri | - | Jimbo la Tumbatu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 32. Mhe. | Haji Shaaban Waziri | - | Jimbo la Uzini |
| 33. Mhe. | Hamza Hassan Juma | - | Jimbo la Kwamtipura |
| 34. Mhe. | Harusi Said Suleiman | - | Jimbo la Wete |
| 35. Mhe. | Hassan Hamad Omar | - | Jimbo la Kojani |
| 36. Mhe. | Hassan Khamis Hafidh | - | Jimbo la Welezo |
| 37. Mhe. | Hudhaima Mbarak Tahir | - | Nafasi za Wanawake |
| 38. Mhe. | Hussein Ibrahim Makungu | - | Jimbo la Mtoni |
| 39. Mhe. | Juma Makungu Juma | - | Jimbo la Kijini |
| 40. Mhe. | Juma Ali Khatib | - | Uteuzi wa Rais |
| 41. Mhe. | Issa Haji Ussi Gavu | - | Jimbo la Chwaka |
| 42. Mhe. | Kombo Mwinyi Shehe | - | Jimbo la Wingwi |
| 43. Mhe. | Machano Othman Said | - | Jimbo la Mfenesini |
| 44. Mhe. | Maryam Thani Juma | - | Jimbo la Gando |
| 45. Mhe. | Mihayo Juma Suleiman | - | Jimbo la Mwera |
| 46. Mhe. | Miraji Khamis Mussa | - | Jimbo la Chumbuni |
| 47. Mhe. | Mohamed Mgaza Jecha | - | Jimbo la Mtambile |
| 48. Mhe. | Mohamed Ahmada Salum | - | Jimbo la Malindi |
| 49. Mhe. | Mtumwa Peya Yussuf | - | Jimbo la Bumbwini |
| 50. Mhe. | Mussa Foum Mussa | - | Jimbo la Kiwani |
| 51. Mhe. | Mwanaidi Kassim Mussa | - | Nafasi za Wanawake |
| 52. Mhe. | Mwantatu Mbarak Khamis | - | Nafasi za Wanawake |
| 53. Mhe. | Mwanajuma Kassim Makame | - | Nafasi za Wanawake |
| 54. Mhe. | Dkt. Mwinyi Talib Haji | - | Mwanasheria Mkuu |
| 55. Mhe. | Nadir Abdullatif Yussuf | - | Jimbo la Chaani |
| 56. Mhe. | Nassor Salim Ali | - | Jimbo la Kikwajuni |
| 57. Mhe. | Nassor Ahmed Mazrui | - | Uteuzi wa Rais |
| 58. Mhe. | Omar Said Shaaban | - | Uteuzi wa Rais |
| 59. Mhe. | Panya Ali Abdalla | - | Nafasi za Wanawake |
| 60. Mhe. | Rukia Omar Ramadhan | - | Jimbo la Amani |
| 61. Mhe. | Saada Ramadhan Mwendwa | - | Nafasi za Wanawake |
| 62. Mhe. | Dkt. Saada Mkuya Salum | - | Uteuzi wa Rais |
| 63. Mhe. | Saidi Saleh Salim | - | Jimbo la Tumbe |
| 64. 5Mhe. | Sabiha Filfil Thani | - | Nafasi za Wanawake |
| 65. Mhe. | Salha Mohamed Mwinjuma | - | Nafasi za Wanawake |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **66. Mhe.** | **Salma Mussa Bilal** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **67. Mhe.** | **Suleiman Makame Ali** | **-** | **Jimbo la Ziwani** |
| **68. Mhe.** | **Suleiman Haroub Suleiman** | **-** | **Jimbo la Kiembe Samaki** |
| **69. Mhe.** | **Sulubu Kidongo Amour** | **-** | **Jimbo la Mkwajuni** |
| **70. Mhe.** | **Shadya Mohamed Suleiman** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **71. Mhe.** | **Shamata Shaame Khamis** | **-** | **Jimbo la Micheweni** |
| **72. Mhe.** | **Shaib Hassan Kaduara** | **-** | **Jimbo la Chake Chake** |
| **73. Mhe.** | **Yahya Rashid Abdulla** | **-** | **Jimbo la Kwahani** |
| **74. Mhe.** | **Yussuf Hassan Iddi** | **-** | **Jimbo la Fuoni** |
| **75. Mhe.** | **Zaina Abdalla Salum** | **-** | **Nafasi za Wanawake** |
| **76. Mhe.** | **Zawadi Amour Nassor** | **-** | **Jimbo la Konde** |

| | | |
|---|---|---|
| **Ndg. Raya Issa Msellem** | **-** | **Katibu** |

**Kikao cha Nane - Tarehe 23 Februari, 2021**

*(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Naibu Spika, (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua*

**TAARIFA YA SPIKA**

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, katika kikao cha Baraza cha tarehe 17 Februari, 2021 Mhe. Nassor Salim Ali aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Nam. 56 na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora aliahidi kujibu swali hilo kwa maandishi. Aidha, katika kikao hicho Mhe. Asha Abdalla Mussa aliuliza swali la nyongeza lililotokana na swali la msingi Na. 46 na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ alihidi kujibu kwa maandishi.

Sasa nawaomba Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ wasome majibu ya maswali ya nyongeza yaliyoulizwa na Wajumbe hao.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Nassor Salim Ali swali lake la nyongeza kuhusu mali na kiasi chafedha kilichorejeshwa serikalini tokea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi baada ya kukamilisha uchunguzi wake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imeanzishwa rasmi mwaka 2013 kupitia Sheria Nam. 1 ya mwaka 2012, Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar tokea kuanzishwa kwake imefanikiwa kuokoa na kurudishwa mali zenye thamani shilingi 850,606,445/= baada ya kukamilisha uchunguzi, kutokana na tuhuma za aina mbali mbali ikiwemo kukwepa kodi, matumizi mabaya ya ofisi na kusafirisha magendo kama inavyoonekana kwenye jaduweli ifuatayo.

Fedha zilizookolewa kuanzia mwaka 2018 hadi 2021 mwaka 2018 ni shilingi 78,387,719/= mwaka 2019 shilingi 275,717,302/= mwaka 2020 shilingi 474,631,424/= na mwaka huu wa 2021 tayari shilingi 21,870,000/= zimeokolewa, taarifa zaidi na maeneo ya undani zaidi yako kwenye kiambatisho ambayo orodha yake ni ndefu sana. Lakini naomba tu nitoe taarifa ndogo kwamba maeneo ambayo yametuhumiwa zaidi ni maeneo ya matumizi mabaya ya ofisi, kukwepa kodi, rushwa katikaajira, ubadhirifu wa mali na mapato, kusafirisha magenzo, matumizi mabaya na mali.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora. Sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa majibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Asha Abdalla Mussa swali lake la nyongeza lililotokana na suala la msingi Na. 46 kama ifuatavyo.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Wakala wa Ulinzi JKU ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni mia sita, hata hivyo Wakala ilifanikiwa kuwasilisha katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali jumla ya shilingi milioni mia tano na hamsini sawa na asilimia tisini na mbili ya makusanyo yaliyopangwa naomba kuwasilisha.

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi:** Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha mezani Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 RE 2020 kwa mujibu wa kifungu cha 132 cha Katiba ya Znazibar ya 1984.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hati mezani Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar mwaka 2020.

**Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa):** Mhe. Naibu Spika, kwa heshima naomba kuweka Hati Mezani Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mwaka 2020.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

### Nam. 87

### Athari Zinazoweza Kusababishwa na Miti Iliyopo Pembezoni mwa Barabara

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed –** Aliuliza:-

Katika barabara kubwa ya kuelekea *Airport* maeneo ya Migombani kuna minazi kama mitano ambayo inahatarisha usalama kwa wananchi wanaopita na vyombo vya moto, minazi ambayo imeshainama kuelekea barabarani na muda wowote inaweza kuanguka.

(a) Je, wizara inafahamu uwepo wa minazi hiyo ambayo inaweza kusababisha madhara.

(b) Je, ni hatua gani zitachukuliwa ili kuzuia kutotokea kwa athari zitakazotokana na uwepo wa minazi hiyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 87 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, napenda kumjuulisha Mhe. Mwakilishi kwamba, ofisi ilikuwa haifahamu uwepo wa minazi hiyo ambayo inaweza kusababisha madhara. Lakini nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kutujuulisha hali hiyo na nampongeza sana kwa juhudi zake hizo, mara baada ya kupata taarifa wizara ilitembelea eneo hilo na juhudi zilichukuliwa za kuhakikisha kwamba minazi hiyo inaondolewa.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa minazi hiyo haipo tayari hatua zimeshachukuliwa za kuiondoa.

**Mhe. Fatma Ramadhan Mohamed:** Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake alizozichukua maana ni kweli hatua imeshafanyika na mimi mwenyewe nimekweda *site* nimeona nawapongeza sana. Pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kuchagua Mawaziri majembe kama haya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pamoja namajibu mazuri na utekelezaji wa Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Napenda nimuulize Mhe. Waziri, je wizara yake inafahamu uwepo wa minazi mingine hatarishi ambayo ipo karibu na kwa Makamu wa Pili wa Rais karibu na *Zanzibar Beach Resort*.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Wizara hivi sasa imo katika hatua za kupitia maeneo yote katika Manispaa ya Mji lakini pia katika Halmashauri za Wilaya mbali mbali ili kuona miti ambayo iko hatarishi hasa katika maeneo ya barabarani na makaazi ya wananchi, suala hilo linatekelezwa kwa mujibu wa sheria ya Serikali za Mitaa *Zanzibar Local Government Authority* No. 7 ya mwaka 2014.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Kaimu Waziri kwa majibu mzuri, lakini naomba kumuuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo.

a) Kwa kuwa amekiri na majibu yake yanaonesha hasa kwamba kunahitaji uratibu nimuulize tu moja kwa moja katika hizi taasisi za Serikali za Mitaa kuna idara gani

inayoshughulikia zoezi hilo la uondoshaji wa ile miti na utaratibu wao wa kupita na kuona hii ni hatarishi.

b) Kwa kuwa mazingira yetu yanaendana na upandaji wa miti pembezoni mwa barabara na zamani tukiona, hatua zipi wakishaondosha lakini kurejesha ile haiba kwa ile miti na kurejesha katika utaratibu mpya watazichukua.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Kwanza chombo kinachohusika ni Mabaraza ya Miji yenyewe na Halmashauri za Wilaya hivyo ndio vyombo vinavyohusika. Nafikiria Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi huwa tunaona kila baada ya kipindi maafisa wanapita wanakagua maeneo hayo, lakini ile miti ambayo inazidi katika maeneo ya barabarani inakatwa na kuondoshwa.

b) Sasa jukumu hili la kurejesha haiba bado liko kwenye Manispaa lakini pia kwenye Halmashauri zenyewe.

**Nam. 92**

**Uhaba wa Majengo ya Madarasa Katika Skuli ya Micheweni**

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis –** Aliuliza:

Kupitia fedha za maendeleo ofisi yako awamu iliyopita iliahidi kukamilisha vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na wadau wengine wa elimu.

Je, ni lini kazi hiyo ya ujenzi itafanyika, ili kuondoa msongamano wa uchache wa nafasi katika vyumba vya madarasa skuli ya msingi Micheweni.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ -** Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swaali lake Nam. 92 na kabla ya kumjibu naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ inatekeleza Mradi wa Maendeleo chini ya ufadhili wa Tume ya Mipango Zanzibar wa kukamilisha vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi. Mradi huu uliasisiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na mara baada ya ugatuzi ulihamishiwa katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Lengo la mradi huu ni kutekeleza ahadi ya

serikali kwamba wananchi watapokuwa wameonesha kwa vitendo jitihada za kujenga vyumba vya madarasa kufikia hatua bado kuezeka tu, basi serikali itakamilisha hatua iliyobakia.

Mhe. Naibu Spika, mahitaji ya kukamilisha madarasa haya yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi ni mengi ukilinganisha na fedha za bajeti tunazopatiwa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha uliopita tulipangiwa kupatiwa shilingi bilioni 1,100,000,000/= lakini hadi mwaka unamalizia Juni 2020 tulipatiwa shilingi milioni 300,000,000/=.

Kwa mwaka huu wa fedha tumepangiwa kupatiwa shilingi bilioni 1,000,000,000 na mpaka sasa tumeshapatiwa shilingi milioni 350,000,000 ambazo tumezitumia kujenga vyumba vya madarasa saba ghorofa ya kwanza katika skuli mpya ya msingi Kwarara kufuatia wadau wengine wa elimu kuishia kujenga sehemu ya chini na serikali kujenga ghorofa ya kwanza yenye vyumba 14, ambapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nayo imejenga vyumba saba na kuifanya skuli hiyo kukamilika na kuwa na jumla ya vyumba vya madarasa 28.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kazi hiyo ya ujenzi wa kukamilisha vyumba vya madarasa vilivyoanzishwa na nguvu za wananchi itafanyika mwanzoni mwa bajeti ijayo ya mwaka 2021/2022, ili kuondoa msongamano wa uchache wa nafasi katika vyumba vya madarasa ya skuli ya Micheweni. Aidha, kwa kuwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (2020 – 2025) imeahidi na kuiagiza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kukamilisha madarasa 1,000 yaliyoanzishwa na nguvu za wananchi, serikali itaongeza fedha za bajeti kuhakikisha maeneo yote Unguja na Pemba yenye madarasa hayo yanakamilishwa.

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yana ufafanuzi wa kutosha na wananchi wa Jimbo la Micheweni wamemsikia, lakini nimuulize swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri ni kweli serikali yetu inajitahidi sana kufuatilia na kama tunavyojua kama wizara imepelekwa kwenye ugatuzi. Lakini nimuulize Mhe. Waziri, ni lini wizara yake imekwenda kwa wananchi wa Jimbo la Micheweni ili kuwatia moyo na wasivunjike moyo ili wajue kuwa watajengewa skuli hii.

**Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ):** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la suala mama kwamba serikali imejipanga kuhakikisha madarasa yote yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yanakamilishwa kama serikali ilivyotoa ahadi kwa wananchi, nilisema hapa katika ilani ya mwaka 2020 hadi mwaka 2025 wizara imepangiwa kukamilisha madarasa elfu moja Unguja na Pemba. Kwa hivyo, nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba wizara yangu itatembelea maeneo yote hayo lakini madarasa yote haya yatawekewa mpango wa utekelezaji, ili ndani ya kipindi cha miaka mitano madarasa yote yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yawe yamekamilika.

**Mhe. Mihayo Juma Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na kunipa fursa yakuuliza swali nyongeza. Kwanza nipongeze majibu ya Mhe. Waziri, lakini vile vile naomba kumuuliza Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Kwa kuwa jitihada za Wizara hii ya Tawala za Mikoa katika suala zima la kusimamia majengo haya inakwenda sambamba na suala zima la kiutawala hasa kugawa shehiya na kwa sasa kuna baadhi ya shehia zimebahatika kukosa kabisa huduma hizi za msingi za skuli katika maeneo hayo, tayari kuna jitihada kubwa ambazo wananchi wetu wamekuwa wakizifanya kwa kushirikiana na viongozi wao.

Je, ni lini sasa Wizara yako na wewe mwenye Mhe. Waziri utakuwa tayari kuja kuona jitihada za wananchi wa shehia ya Masingini ambao tayari wameshajenga vyumba vya madarasa karibu 18 kwa lengo la kuwapunguzia usumbufu watoto wao.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kwa niaba ya serikali nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Mwakilishi, lakini pia kuwapongeza sana viongozi na wananchi kwa shehia ya Masingini kwa kujenga madarasa 18, wizara yangu itatembelea eneo hilo lakini licha ya kusema kwamba tutatembelea bado juhudi za wananchi zitaendelea kuheshimiwa na kama ulivyo utaratibu wa serikali basi nguvu ya serikali nayo itawekeza katika madarasa hayo kumi na nane kwa ajili ya kumalizia shughuli hiyo.

**Mhe. Ameir Abdalla Ameir:** Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Kwa kuwa msimu wa mvua unakaribia na Skuli ya Magogoni Msingi ina hali mbaya ya ukuta kutaka kuanguka muda wowote. Je, lini Mhe. Waziri na timu yake wanaweza kutembelea apale kwa ajili ya kuiokoa ile hali kabla ya msimu huu wa amvua haujafika.

(b) Skuli ya Sekondari ya Mwanakwerekwe "C" nayo ina tatizo kubwa la uvujaji inawezekana kipindi kijacho ch mvua skuli ile ikashindwa kukalika. Sasa kuna hatua gani Mhe. Waziri na hatua zako na timu yako kuweza kuitembelea ile shule kabla msimu wa mvua ambazo zimeanza hivi sasa karibuni kuanza kuweza kulitatua tatizo hili. Mhe. Naibu Spika, Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ):** Mhe. Naibu Spika naomba kumjibu Mhe. Ameir Abdalla Ameir swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwanza nimhakikishie Mhe. Mwakilishi, Waheshimiwa Wajumbe pamoja na wananchi kwa jumla kwamba wizara yangu, inaelewa kwamba iko changamoto ya miundombinu si kwa eneo la Magogoni tu lakini katika maeneo mengi. Changamoto hiyo itatuliwa na juhudi hivi sasa

inafanyika ya kufanya tathmini ya kina kwa maskuli yote Unguja na Pemba kujua ni aina gani ya uharibifu uliokuweko kama uvujaji, kama ukuta kukaribia kuangua na baada ya kupata tathmini hiyo sasa hatua za kurekebisha hali hiyo zitachukuliwa kwa mashirikiano na viongozi wa maeneo hayo pamoja na wananchi.

**Nam. 73**

**Uwekezaji wa Nje wa *(Fdis)* Katika kwa Mwaka 2015-2020**

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum -** Aliuliza:-

Kwa mujibu wa taratibu za uwekezaji kwa wawekezaji wa nje wanatakiwa kutoa huduma kwa jamii inayowazunguka katika eneo la uwekezaji analoekeza.

Je, ni kiasi gani kimetumika na katika maeneo gani kutokana na uwekezaji mbali mbali hususan wa nje (*FDIs*) kuingia katika huduma za kijamii *(Corporate Social Responsibility)* katika kipindi cha mwaka 2015 – 2020.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 73 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, suala la ***"****Corporate Social Responsibility*" kwa miradi ya uwekezaji hadi sasa limekuwa ni suala la hiyari na halijawekewa sheria wala mpango maalum wa kuliratibu, hivyo haitakuwa rahisi kwa sasa kutoa takwimu sahihi. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti wa *'Private Capital Flows'* uliofanywa mwaka 2018 – 2019 jumla ya dola 39.4 milioni zilitolewa kwenye masuala ya ulinzi na usalama na mwaka 2017 jumla ya dola 805,500 zilitumika katika eneo la barabara. Muyuni Hotel na *SPA* wamesaidia kiasi cha shilingi milioni 11,800,000/- kwa kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama katika vijiji vya Mtondoo Jeuri na Mawe Matatu.

Mhe. Spika, pia, baadhi ya jamii zilizo karibu na miradi ya uwekezaji zinanufaika na zinaendelea kupata manufaa na uwekezaji huo. Mfano ujenzi wa Skuli ya Sekondari ya Bwefum; Hoteli ya *Sea Cliff* iliopo Kama imesaidia ujenzi wa Skuli ya Kama na Kiomba Mvua na Wananchi wa vijiji vya karibu wanapata huduma za afya katika hoteli hiyo. *Manta Resort* wameanzisha *NGO 'Kwanini Foundation'* ya Kuhifadhi Mazingira na imeajiri watu 10; wamejenga madarasa 2 katika Skuli ya Kijiji cha Mnarani na kuunganisha mabomba ya maji katika kijiji cha Jiwe Moja na Kijini.

Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kuelewa umuhimu wa *corporate social responsibility* katika kuchangia maendeleo ya nchi na jamii inakusudia kutunga Sheria ya Usimamizi wa masuala ya Utawala Bora ambayo itahusisha usimamizi na uratibu wa masuala ya ***"****corporate social responsibility"*. Pale ambapo sheria hii itakapokamilika mpango wa uratibu utafuata na itakuwa wepesi kupata taarifa na takwimu sahihi juu ya mchango wa wawekezaji katika jamii.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake...

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa punguzeni minongóno nyuma huko.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salimu:** Mhe. Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza:

(a) Ni kwamba pamoja na faida zinazotakana na uwekelzaji zikiwemo ajira kwa jamii inayohusika lakini vile vile jambo jengine muhimu ambalo linazingatiwa katika uwezekaji wa nchini pamoja na *corporate social responsibility*. Sasa masikitiko yangu ni kuona kwamba hadi leo serikali haina utaratibu maalum wa kusimamia *corporate social responsibility* kutokana uwekezaji na hivyo, kufanya uwekezaji huu mara nyengine kuwa na *resistance* kutokana na jamii.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri pamoja na kwamba serikali inaleta sheria ya masuala ya utawala bora sijui kuna *link* gani baina ya utawala bora na masuala ya *corporate social responsibility*. Lakini ninachokiona ni kwamba sheria hiyo ni kwa ajili tu ya kupata taarifa na takwimu sahihi juu ya hiyo michango.

Je, lini sheria hii italetwa na kama inahusisha vile vile katika mikataba, yaani kuwaomba wawekezaji katika mikataba yao kuingiza kifungu cha *CSR*, ili kupata faida kubwa zaidi kwa jamii inayozunguka ule uwekezaji, lini hiyo sheria itakuja hapa katika Baraza la Wawakilishi kwa sababu tunachokiona kwamba *flow* inaongezeka.

(b) Mhe. Waziri anafahamu kwamba baadhi ya maeneo ya uwekezaji wananchi mbali ya kuwa hawafaidiki kutokana na uwekezaji lakini ule uwekezaji unaleta hasara kwa wananchi wengi. Kwa mfano Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni jana alizungumzia kuhusiana na hoteli ambazo zipo katika eneo lake, zinazomwaga maji yale yanayotumikia kwa *swimming pool* kwenye maeneo yake ambayo wananchi wanafanya uvuvi wa mwani *particular*.

Sasa hili sijui kama Mhe. Waziri analifahamu na kama halifahamu yeye anatupa *commitment* gani kufuatilia kuona kwamba uwekelzaji katika maeneo yote wananchi wanafaidika na hawali hasara kutokana na huo uwezekaji ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Mhe. Spika ahsante sana kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum maswali yake kama ifuatavyo:-

Kwa vile sasa hivi hatuna sera au sheria ambayo ina-*guide* masuala ya *corporate social responsibility* wizara yangu imeona umuhimu wa kulilta hili jambo mezani na kuandaa vikao vya *stakeholders*, ili kuweza kupata maoni yao jumuishi, ambayo yaonesha hasa namna gani ambavyo tunataka wawekezaji hawa wawajibika katika *CSR*. Katika hili, labda niseme tu kwamba tunatakiwa tufanye mageuzi makubwa katika namna gani ambayo tunawajibisha hawa wadau wetu, sio tu kwa kuangalia masuala labda ya kuekeza kwenye skuli au hospitali, lakini kuwawezesha wale wanajamii wenyewe kuweza kushiriki katika shughuli za kimaendeleo ya

zile jamii ambazo zinawazunguka lakini vile vile uwa-*empower* kiuchumi kwa maana ya kutengeneza ajira.

Tunafahamu kwamba mahoteli mingi *supply* ya vitu vyzao kwa mfano mboga mboga, matunda na nini wanaagiza kutoka nje, maji wanaagiza kutoka nje. Sasa aina nyengine ya *corporate social responsibility* kuhakikisha kwamba vitu ambavyo vinaweza kupatikana katika ile jamii vitoke pale pale katika ile jamii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sheria ambayo itakuwa tunakuja nayo inakuwa ni *comprehensive* ambayo itakuwa ni jumuishi lakini ita-*focus* zaidi hii *empowerment* ya zile zaidi badala ya kuweka hivi viatu ambavyo tumezowea siku zote vya maji na madarasa na madawati.

Kuhusu *timeline* nafikiri hii itategemea zaidi na mikutano ambayo tutakuwa nayo na *stakeholders*, lakini niseme tu kwamba ni mapema iwezekanavyo *atleast* kabla hata hatujaanza kwenye kusoma bajeti yetu mwezi wa Juni basi huo mswada tuwe tumeshauleta.

Kuhusu athari hasi ambazo zinatokezea ili kwa kweli tunalitambua na maafisa wetu wa Idara ile ya Usalama na Afya kwa maana ya *HOSH* wao ndio wajibu wao mkubwa sana kufuatilia, pamoja na wenzetu wa mazingira kuhakikisha kwamba kuna *compliance* katika masuala ya utunzaji wa mazingira na kwamba muwekezaji anafuta vile vigezo vyote ambavyo tunamtaka aviongeze.

Kwa hivyo, hapa ni kutulia mkazo tu kwa maafisa wetu kuendelea kutekeza wajibu wao kwa kuwafatilia na kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanalindwa na kwamba hakuna athari hasi ambazo zinatokezea katika jamii.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Mhe. Naibu Spika, ahsante kwanza nianze kwa kuipongeza serikali yangu kwa jitihada mbali mbali wanazochukuwa kuhusiana na suala la uwekezaji nchini, lakini nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu mazuri ya serikali, sasa pamoja na majibu hayo naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vitoto (a) na (b) kama ifuatavyo:

Pamoja na kwamba amekiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba hadi sasa hakuna sera wala sheria inayohusiana na miradi hii ya *CSR*, lakini atakubaliana na mimi kwamba wapo baadhi ya wawekezaji nchini ambao katika mikataba yao ya ukodishwaji wa ardhi au ya umiliki wa ardhi imeainishwa ndani ya mikataba na wamepata punguza la kodi ya serikali takribani dola laki nne kwa ajili ya kutekeleza miradi hii ya jamii.

(a) Sasa nataka kumuliza Mhe. Waziri analifahamu kwa kiwango gani suala hili.

(b) Nini *commitment* ya serikali kwa wawekezaji ambao wamekiuka mikataba ya uwekezaji hasa katika utekelezaji wa miradi hii *CSR* nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Mhe. Spika, naomba arejee swali la pili nini *commitment* ya.

**Mhe. Shaaban Ali Othman:** Mhe. Naibu Spika, nataka kujua nini *commitment* ya serikali kwa wawekezaji ambao wamekiuka matakwa ya mikataba yao ambapo ndani ya mikataba husika imeanishwa na wamepata punguzo la kodi ya serikali kwa ajili ya utekelezaki wa miradi hiyo nini *commitment* ya serikali kwa wawekezaji wa aina hiyo.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:** Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Shaaban Ali Othman swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mwekezaji wanapokuwa wamepewa eneo kwa ajili ya kuliendeleza kuna maalum ambao tunakuwa tumempa na suala hilo ambalo unaligusia wewe la punguzo la kiasi cha dola laki nne nafikiri unagusia mradi ule wa *Pennyroyal* ambao muwekezaji aliomba kama kupewa *Strategic Investment Status* kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi ilitambua hilo la kumpatia hilo punguzo. Lakini bahati mbaya sana kwamba muwekezaji huyo bado mpaka sasa hivi amekosa kuliendeleza lile eneo kama inavyostahiki.

Sasa kwenye *commitment* ya serikali kwa kweli kuendelea kuwabana hawa wawekezaji na kuhakikisha kwamba wanafuata au wanatekeleza ule wajibu wao kama ambavyo imeanishwa katika mikataba. Sheria kwa sasa hivi inakupa miezi sita kuliendeleza eneo na kama hujaliendeleza ndani ya kipindi hicho basi tuna haki kama serikali yakuja kulichukua na kuli-*reassign* kwa mtu mwengine.

Kwa hiyo, ni kiritu kwamba umefika wakati muafaka sasa kwamba tufanye uhakiki ambao unastahiki kuyapitia haya maeneo, na kwa wale watu ambao bado wanashindwa kuyaendeleza licha ya kwamba tumetoa zile *incentives* zote ambazo zinatakiwa wakishindwa kuwajibika, basi serikali ichukuwe hatua stahiki kuyachukuwa yale maeneo kuya-*reassing* na kuwepa wawekezaji wengine ambao wana dhamira ya kuweza kuyaendeleza. *(Makofi)*

**Nam. 64**

**Kuimarika kwa Maslahi ya Walimu**

**Mhe. Habib Ali Mohamed -** Aliuliza:-

Walimu ni kioo cha jamii. Hali hii imepotea katika tawala nyinyi zilizopita na kupelekea walimu kutokuwa na hadhi.

Je, serikali ina mpango gani juu ya suala la kuwaongeza mishahara walimu jambo ambalo waziri aliyepita na serikali walishindwa kufanya hivyo.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake Nam. 64 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, napenda kulijuilisha Baraza lako tukufu kwamba, sio sahihi kama waziri aliyepita pamoja na serikali iliyopita ilishindwa kuongeza mishahara kwa walimu na wafanyakazi wengine. Azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wakiwemo walimu wanaongezewa mishahara na kupatiwa maslahi mengine kila hali ya uchumi inapoimarika.

Aidha, Serikali ya Awamu ya Saba iliyoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais Mstaafu na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliongeza mishahara ya walimu na wafanyakazi wengine mara sita katika vipindi tofauti vya uongozi wake. Hivyo, serikali hii ya awamu ya nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, haitosita kuongeza mishahara ya walimu pale hali ya uchumi wa nchi yetu itakaporuhusu na serikali itakapoona haja ya kufanya hivyo.

**Mhe. Habib Ali Mohamed:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Elimu nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna upungufu wa walimu wa sayansi katika baadhi ya maskuli na serikali ya awamu ya nane imejipanga kuwekeza katika viwanda, kupata ma-*specialist* katika mahospitali. Je, serikali ina mkakati gani wa kuongeza walimu wa sayansi katika maskuli ambayo hayana walimu wa sayansi wa kutosha.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake la nyongeza kama ifuataavyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la kusomesha ni jukumu la serikali ambalo tumekuwa tunalibeba tangu mapinduzi matukufu. Kwa sasa kwa upande wa elimu wa upande wa Zanzibar kwa Sekta ya Elimu tunayo mapungufu katika masomo ya hesabu na fizikia hasa katika changamoto hii, lakini changamoto hii hapo tu kwa upande wa Zanzibar hata duniani kote mara nyingi wanafunzi wengi na ile *interest* au ile hamu katika masomo ya hesabu. Lakini serikali yetu sasa kwa kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunasomesha walimu sasa hivi karibia mia nne katika vyuo vyetu, lakini hawa ndio tunaowabadilisha waliokuwa katika masomo ya sanaa kusomea masomo ya sayansi kupitia mradi wa *ZISPP*.

Lakini pia hali kadhalika tunazidi kuhamasisha walimu ambao watakaosoma kuwapa *incentive* tofauti au mafao ili waweze kuingia katika masomo ya sayansi. Kwa hivyo, hii kupitia Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi wazidi kuhamasisha katika maeneo yao, kwa sababu ndio mabalozi nambari moja wa elimu kwa upande wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sababu wao ndio wawakilishi wa wananchi.

Kwa hiyo, tushirikiane kwa pamoja sote baina ya serikali pamoja na wawakilishi katika kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu ambao wanakwenda kusomea elimu basi jitihada zinakuwa ni zuri kabisa, ili tuweze kuwasaidia watoto wetu ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, lakini nimpokeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake kwenye swali mama alijibu mwisho kabisa kule Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dkt. Hussein Ali Mwinyi Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi haitosita kuongeza mishahara pale hali ya uchumi itakaporuhusu au serikali inapokuwa inaona ipo haja ya kufanya hivyo.

Mhe. Waziri kwa kuwa hapa pana haki na stahiki za kiutumishi kwa walimu na wafanyakazi wengine lakini mimi nazungumza zaidi hawa walimu ambao waliguswa hapa. Je, tushike lipi katika kauli hizi mbili maana pana kauli hapo uchumi utakaporuhusu au serikali itakapoona kuna haja ya kufanya hivyo. Je, kiutumishi tushike lipi hapa serikalini itakapokuwa na uwezo au itakapojisikia kufanya hivyo lipi tushike maana pana kauli mbili.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe, Naibu Spika, kwanza niseme kwamba hapakuwa na kauli mbili, kauli ni moja tunapozungumza suala la uchumi tunazungumzia mapato ya serikali ambayo inajipanga kwa kila mwaka ambayo inataka kutumia. Tunapoangalia sasa hivi dunia inapita katika kipindi kigumu hasa kutokana na maradhi ya *Covid 19* (*Corona*). Kwa hiyo, serikali inapojipanga bajeti yake tunaangalia katika mpango kama ambavyo jana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango alipofanya majumuisho ya hotuba yake na sisi tunaposema kwamba katika kuongeza maslahi au mafao au mishahara ya wafanyakazi hatuangalii tu katika sekta ya elimu, kuna sekta ya afya, kuna sekta ya ujenzi na maeneo mengine. Kwa hiyo, tunaposema hali kila itakaporuhusu maana yake tunazingatia maeneo yote ambapo serikali inahudumia kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, jana tulizungumza hapa suala la umuhimu wa elimu, suala la afya pamoja na maji katika mambo ambayo yanawagusa wananchi kila siku. Kwa hiyo, sisi kwa upande wa serikali tuko kwenye mipango yetu hatukurupuki wala haturushi mkuki gizani, tunafanya mambo kwa mpango ndio azma ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kupata nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali dogo tu la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri akubaliane na mimi kwamba miongoni mwa changamoto zinazowakabili walimu ikiwemo ni uhaba wa mshahara kama alivyosema kwenye jibu lake mama, lakini na changamoto mzima ya usafiri kwa wale walimu wanaosomesha maeneo ya mbali. Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwapa nauli lakini nauli hizo huwa zinacheleweshwa na wengine hawapewi kabisa. Je, wizara haioni kwamba kuna haja sasa hivi ya kuwapa angalau kitambulisho waweze kutambulikana kwenye usafiri. Nakushukuru.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ushauri wake wa vitambulisho tumeuchukua. Lakini niseme tu kwamba changamoto katika malipo hutokezea pale ambapo taarifa za mwalimu wakati mwengine zinagongana wanapokuwa wapo wizarani, lakini pia inategemea na mpango wakati mwengine hutokezea fedha kuchelewa kuingia Wizara ya Fedha kutokana na mazingira.

Lakini tunajitahidi kama serikali kuhakikisha kwamba walimu tunawatambua katika maeneo muhimu, na kwa kipindi hiki tunatambua kwamba hili suala la ugatuzi limeleta aina ya

changamoto, ndio maana hata jana tulipozungumza tulisema kuwa serikali hii inakusudia kufanya tathmini kwa ujumla juu ya suala zima la ugatuzi katika eneo la elimu, afya na kilimo kwa pamoja. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 65**

**Usahihishaji wa Mitihani ya Kidato cha Nne na Sita**

**Mhe. Habib Ali Mohamed** - Aliuliza:-

Uwiano katika shughuli ya usahihishaji mitihani ya kidato cha nne na sita limeegemea zaidi upande wa Tanzania Bara kuliko Zanzibar.

Je, serikali ina mkakati gani ya kuhakikisha ongezeko la walimu wa kusahihisha mitihani kutoka Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 65 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kulijuisha Baraza lako tukufu kwamba suala la kusahihisha mtihani wa taifa ni suala nyeti sana linalohitaji walimu wenye sifa, nidhamu na uzalendo wa kutunza siri kwa maslahi ya kazi na taifa. *NECTA* huchagua walimu kwa kuzingatia vigezo hivyo na si kwa kuangalia uwiano wa kiusawa wa walimu katika maeneo wanayotoka. Kwa upande wa Zanzibar, *NECTA* kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali huchagua walimu wa masomo tofauti ambapo kwa mwaka 2020 jumla ya walimu 580 kutoka Zanzibar walishiriki katika zoezi la kusashihisha mitihani ya kidato cha nne na sita. Ahsante sana mheshimiwa.

**Mhe. Habib Ali Mohamed:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri aliyoyatoa, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika mwaka 2020 jumla ya walimu 580 walikwenda kusahihisha mitihani ya *NECTA* ya kidato cha nne na sita. Je, ni walimu wangapi waliotoka katika kisiwa cha Pemba.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Habib Ali Mohamed swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, sifa za walimu zinakuwa zimeanishwa katika usahihishaji wa mitihani hii kutokana na utaratibu wa kanuni ambazo zimepagwa na *NECTA*, na sisi kwa upande wa Serikali ya Zanzibar wakati wowote ambapo tunakuwa tunajipanga kwa haya tunazingatia kwa pande zote mbili, kwa upande wa Zanzibar lakini pia kuangalia upande wa Pemba.

Kwa mfano, katika mitihani ya kidato cha nne, la pili na darasa la nne na la sita tulikuwa tuna walimu 927 kwa pale ni 304 na 706. Suala la kwamba kujua idadi maalum kwa upande wa Pemba mimi nafikiri Mhe. Naibu Spika, hili nitampatia Mhe. Mwakilishi idadi hii kwa maandishi ikiwa kuna umuhimu huo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Bihindi Hamad Khamis:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kaeleza kuwa alikuwa hawajui idadi ni wangapi lakini je wanawake ni wangapi Unguja na Pemba.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Bihindi Hamad Khamis swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, nafikiri swali hili la nyongeza na lile lilopita linafanana sana kwa sababu takwimu wanayoitaka wao ni ya idadi ya wanaume pamoja na wanawake. Nafikiria hili kwa umuhimu wake Mhe. Mwakilishi basi nitampatia la miaka mitano au mitatu kwa maandishi itamsaidia pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi. *(Makofi)*

**Mhe. Miraji Khamis Mussa:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, lakini nimshukuru Mhe. Waziri japokuwa katika majibu yake yale ya mwanzo yana ukakasi kidogo, maana sisi tunaishi na walimu katika majumba yetu na hawajawahi kwenda kusahihisha mitihani. Sasa kuna maelezo ameyatoa Mhe. Waziri kwa suala hili linahitajia walimu wenye sifa, nidhamu na uzalendo wa kufanya kazi hii.

a) Je, unathibitishia kwa sababu wengine hawajawahi kwenda ndio hao waliokosa nidhamu katika wizara yako na uzalendo.

b) Kama wapo walimu wa aina hii utawachukulia hatua gani kwa sababu tumeona wanarejea wale wale maana na walimu kukosa nidhamu ni jambo moja halistahiki kwenye jamii yetu na uzalendo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ni jambo la msingi sana tunapozungumza suala la walimu, walimu kwanza ni kioo katika jamii kama tunavyohamu. Tunaposema kuhusu sifa tunazungumzia kwa sababu suala lenyewe kama nilivyosema mwanzo katika majibu ni suala nyeti la kwenda kusahihisha linahitaji nidhamu maana yake ina maana wao wenyewe katika mapendekezo walimu huchaguana pia kwa sababu si jambo ambalo kama wizara tunachagua sisi. Mapendekezo haya hutokana na mtu ambapo kama alivyo katika maeneo husika tuna kamati za skuli, tuna viongozi ambao ni wa kijamii kwenye maeneo husika.

Mhe. Naibu Spika, katika swali hili inawezekana suala la uzoefu ni suala la msingi huwezi ukampeleka mtu leo ukamfundisha jambo la msingi la kusainisha mitihani, mwaka ujao pia ukamuondoa ili kwa sababu yule mtu apate posho. Sisi tunataka ukiangalia kwamba ile kazi inafanyika kuliko kuweka suala la posho mbele, na hili ni jambo ambalo sasa hivi sisi kwa upande wa serikali tunaliangalia sana.

Kwa hiyo, umuhimu wa mtu kufanya kazi kwa uadilifu ni suala la msingi, na inawezekana pengine Mhe. Mwakilishi katika eneo lake labda anaye mtu mwalimu au analo jina ambalo anahisi yeye mtu yupo makini na anastahiki pia akaweko katika orodha basi mimi kwa upande wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali sitasita kupokea jina hilo au watu ambao yeye anahisi wataweza kutusaidia. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 77**

**Walimu Kutokulipwa Posho la Nauli**

**Mhe. Bakar Hamad Bakar** - Aliuliza:-

Miongoni mwa haki zinazopaswa kutolewa kwa walimu ni posho la nauli (*bus fair*). Hata hivyo, posho hili halilipwi ipasavyo kwani baadhi ya walimu hulipwa mara mbili, wengine hulipwa kwa upungufu na wengine hawalipwi kabisa.

(a) Je, ni vigezo gani vinavyotumika katika kuwalipa walimu posho lao hilo.

(b) Je, serikali imechukua hatua gani kuhakikisha haki za walimu hawa zinapatikana kwa wakati.

**Mhe. Waziri Elimu na Mafunzo ya Amali** - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 lenye kifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, nauli hulipwa kwa fedha za matumizi ya kawaida na sio kutoka kwenye mishahara, pia kupitia toleo la serikali la barabara, nauli inalipwa kwa kuzingatia masafa ya mwalimu kutoka anapoishi mpaka katika kituo chake cha kazi, ukitoa nauli ya kawaida ya daladala. Hakuna mwalimu anayelipwa mara mbili, isipokua wale wenye vyeti tu ambao wanasomesha sekondari tunawalipa posho la kufundishia na usafiri kwa wale wanaosomesha skuli za mbali zenye masafa yanayostahiki kulipwa nauli. Kwa sasa walimu wanadai nauli za miezi miwili tu ya Oktoba na Novemba, 2020 deni ambalo tulishaliorodhesha Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kama tunavyotakiwa kufanya.

(b) Wizara huorodhesha majina ya walimu kila mwezi na kuwasilisha Ofisi ya Utumishi na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuwapatia walimu haki zao zikiwemo za maposho na nauli. Utaratibu huu hufanyika kwa wakati ila kuna changamoto za upatikanaji wa fedha kutoka katika taasisi husika. Wizara itahakikisha changamoto za walimu za kudai haki zao zinapatiwa ufumbuzi wa kudumu ili na wao kuwajengea imani na ari ya kufanya kazi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme wazi kwamba sijaridhika na majibu hayo ya Mhe. Waziri na kwa sababu sisi wenyewe tunaishi na walimu huko ambako tunaishi, wapo walimu wanadai zaidi ya miezi nane. Kuna walimu kwa mwaka 2020 wamelipwa miezi miwili tu na walimu hawa wanastahili kulipwa posho zao hizi. Sasa majibu ya Mhe. Waziri hapa anasema ni miezi miwili tu ambayo wanadaiwa, mimi nimuombe Mhe. Waziri na namuuliza je yupo tayari kulifuatilia suala hili kwa kina na kuleta majibu hapa Barazani ambayo yanaridhisha.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Bakar Hamad Bakar swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika,

katika majibu mama ambayo nimeyatoa kwamba sisi kwa upande wa serikali nilisema kuwa tunaheshimu na tunaamini walimu ni kioo katika jamii na kila pale hali inaporohusu katika maliimbikizo tofauti tunahakikisha kwamba zile fedha ambazo wanatakiwa walipwe katika posho zao na maslahi tunazingatia.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu takwimu hata katika likizo za huduma kutoka mwaka 2021 hadi leo kila mwaka tunakuwa tunaweka fedha tofauti. Mwaka 2011 tulilipa milioni 11,500,000/=, mwaka 2012 tulilipa milioni 224,200.000/-, mwaka 2013 tumelipa milioni 280 katika awamu mpaka tunafika mwaka 2019. Lakini katika fedha hizi na posho inawezekana kwamba yapo mapungufu ambapo yametokea katika aidha mwalimu husika au katika eneo husika.

Mhe. Naibu Spika, mwanzo nilisema katika suala zima la ugatuzi kuna changamoto nyingi zilijitokeza kwa walimu wetu baina ya kupeleka majina kutoka wizarani pamoja ni wizara ambayo ni dhamana kwenye Tawala za Mikoa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kama una mwalimu ambaye yeye anadai haki zake au walimu katika eneo lake tusisubiri mpaka tuje katika Baraza la Wawakilishi hapa kuuliza maswali. Sisi kama serikali tunafanya kazi kila siku wizara yetu ipo na nawapongeza sana waheshimiwa kila siku mbili tatu wananitumia message kutafuta haki za walimu. Kwa mfano, Mhe. Mwakilishi kutoka Bumbwini nampongeza sana kwani kila mara ananiletea tusisubiri sisi kuja Barazani kubonyeza na kukumbushia suala la mwalimu mmoja, wawili au wengine. Mhe. Naibu Spika, jambo la msingi tunalichukua na sisi tutalifuatilia kulifanyia kazi tukiamini kwamba kushirikiana ni njia moja muhimu sana baina ya sisi na nyinyi wawakilishi wa wananchi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Shabaan Ali Othman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Waziri napenda nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu swali la msingi limezungumzia haki za walimu, moja kati ya haki ambazo wanastahili walimu hasa wa Zanzibar ni kupata fursa sawa hasa ya kwenda kusahihisha mitihani. Mhe. Naibu Spika, katika majibu yake ya maswali yaliyotangulia Mhe. Waziri alielezea uwepo wa sifa na kukosekana kwa sifa ndio kuna sababisha nani aende nani asiende.

Je, ni lini sasa serikali kupitia wizara yake itakuja na mwongozo mahususi utakaoainisha vigezo na sifa stahiki ambao utatoa fursa sawa sasa kwa walimu wote Zanzibar nzima kupata kujielewa wanakidhi kiasi gani kupata haki yao hii ya msingi.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, swali hilo sio swali la msingi ingawa kawaida kama Mhe. Waziri ataweza kulijibu basi nitampa fursa hiyo alijibu, lakini kama anakataa kujibu kwa sababu ni swali la msingi na ningemuomba mheshimiwa ulilete zaidi kama ni swali la msingi.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Shabaan Ali Othman swali lake la nyongeza, kama ulivyosema kwamba halikuwa katika swali mama lakini nitajitahidi kadri ya uwezo wangu kuweza kumpa majibu kwa sababu yeye ni mwakilishi wa wananchi na ana hamu kupokea majibu katika maeneo tofauti.

Mhe. Naibu Spika, suala alilolizungumza Mhe. Mwakilishi miongozo ipo katika wizara, serikali inaongozwa kwa mujibu wa sheria pamoja na sera ambayo tumejiwekea sisi ya elimu katika 2006. Jibu ambalo nililotoa awali ni katika suala ambalo tunashirikiana na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kwenye *NECTA*, na mwongozo huu umepangwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi tunashirikiana nao katika majibu ambayo niliyotoa.

Mhe. Naibu Spika, ikiwa kama anakusudia kwamba sisi tuwe tunatoa matangazo kwa upande wa SMZ kwa wale walimu ambao wanatoka Zanzibar, nalichukua hili kama ushauri siwezi kumwambia moja kwa moja tutashirikiana na wenzetu, ili kuhakikisha kwamba hizi fursa ambazo anataka wa Zanzibar walimu wote wazisikie, basi tutalifanyia kazi. Lakini nimuhakikishie tu miongozo yote na sifa tayari ipo kama nilivyosema mwanzo na huu ndio utaratibu wa kiserikali. Serikali inaendeshwa kwa mujibu wa sheria na sisi tunafuata miongozo ambayo yote tunapanga kwa kushirikiana na wenzetu wa pande zote mbili za Muungano. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, na nachukua fursa hii sana kumpongeza Mhe. Waziri *basically* anakuwa *very responsive* hata ukimtumia *message* kuhusiana na masuala ya walimu amekuwa akijibu na amekuwa akifuatilia. Lakini nimekuwa *worried* Mhe. Naibu Spika kwamba maswali yaliyokuwa yakitoka hapa kama kuna hizi changamoto ambazo zinatokea kwa walimu, Mhe. Waziri anajaribu kutuaminisha au kutwambia kwamba kama kuna hizo changamoto yeye tumpelekee, *actually* sio kazi yake.

Sasa nilikuwa nataka tu kujua kama mifumo iko imara amezungumza kwamba utaratibu na mifumo iko imara. Ni hatua gani tunazichukua kwa hao ambao wanahusika na utekelezaji wa hii miongozo ambayo inatolewa na bado wakawa hawawajibiki mpaka inatufanya sisi kila siku tumtumie *message* Mhe. Waziri na yeye aanze kufuatilia badala ya kusimamia Sera ya Elimu. Hatua gani zinachukulia kwa wanaohusika na wakawa hawawajibiki mpaka hizi changamoto za walimu zikawa zinatokea. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum swali lake la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwanza serikali hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria kama nilivyosema na tunaongozwa kwa Sheria ya Utumishi wa Umma juu ya wafanyakazi wote ambao ni watendaji wetu. Kuna wale ambao wanakuwa ni wateule wa Mhe. Rais kuanzia ngazi ya Mawaziri kuja Makatibu Wakuu na Wakurugenzi. Sasa kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria hawa wote katika ngazi hii wanawajibika kwa Mhe. Rais pamoja na serikali nzima kwa ujumla kwa sababu yeye ndiye kiongozi mkuu.

Mhe. Naibu Spika, na sisi ambao tunamsaidia Mhe. Rais kazi yetu ni kuhakikisha katika wizara zetu na wasimamizi wote kutoka Katibu Mkuu na wengine wanafanya kazi kwa mujibu wa sheria lakini pia kwa mujibu wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na hotuba ambayo Mhe. Rais ameitoa hapa na hotuba nyenginezo.

Sasa katika yale ambayo alisema kwamba serikali katika awamu hii labda kuna hisia kwamba kuna maeneo mengine mambo hayajakaa sawa. Kwa kweli, nafikiri aendelee kuwa mvumilivu

lakini sisi kwa upande wa serikali tunajipanga kwamba haya yote tuweze kuyaondoa. Safari yoyote ni hatua, mwanzo wowote lazima katika mabadiliko wengine watakuwa hawako tayari, wale ambao watakuwa hawako tayari jibu lake ni moja tu ni kutumbua na mwenyewe analifahamu hili, ukiharibu ina maana wewe hutaki kuwa katika safari hii au basi hili maana yake utakuwa unaturudisha nyuma.

Mhe. Naibu Spika, sisi tutasimamia na niwaahidi Waheshimiwa Wawakilishi kwamba sisi sote kwa upande wa serikali *speed* tulioanzanayo hii haitarudi nyuma na tutakwenda nayo sasa hivi moja kwa moja, tayari Mhe. Rais ameunda serikali tuna Makatibu Wakuu naamini wale wakurugenzi wote waliokuwepo sasa hivi sidhani kama kila mmoja atabakia katika nafasi yake, mabadiliko yapo. Kwa hivyo, naamini kwamba mageuzi yatakuwepo na tutasimamia na tutafanya kazi kwa mashirikiano, lakini kwa *speed* zaidi. Haya yote aliyoyasema nayakiri na tutayachukua tutayafanyia kazi katika usimamizi wote. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 89**

**Ukosefu wa Maji Safi na Salama katika Baadhi ya Maeneo ya Micheweni**

**Mhe. Shamata Shaame Khamis** - Aliuliza:-

Jimbo la Micheweni ni miongoni mwa eneo ambalo bado huduma ya maji upatikanaji wake ni wa shida sana hasa kwa baadhi ya vijiji vilivyomo ndani ya jimbo, licha ya jitihada za serikali zinazoendelea kufanyika.

(a) Je, wizara inalifahamu tatizo hilo kwa undani wake.

(b) Je, ni lini kadhia hiyo itaondoka ili wananchi wetu waendelee kufaidika na huduma zinazotolewa na serikali yao.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini** – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 89 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, maeneo yote ya Micheweni kwa ujumla yanapata huduma ya maji katika vijiji vyake vyote vitano ambavyo ni Shumba Mjini, Micheweni, Mjini Wingwi, Kiuyu na Maziwang'ombe.

Aidha, kuna vijiji ambavyo vinapata huduma ya maji kwa ukamilifu kila siku mfano Shumba Mjini, Chamboni na Kwale na baadhi ya vijiji vinapata huduma ya maji kila siku kwa upungufu mfano vijiji vya Majenzi, Mjini Wingwi, Kiuyu na Maziwang'ombe.

(a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu inalifahamu suala la hali ya maji katika eneo la Micheweni kwa undani wake. Pia, wizara inayafahamu maeneo yote yanayopata huduma za maji kwa upungufu.

(b) Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Mamlaka ya Maji ina dhamira kubwa ya kuliondosha tatizo la maji katika vijiji vyote vya Micheweni. Dhamira hiyo ni pamoja na kuongeza mabomba ya maji katika maeneo ambayo hayajafikiwa na mabomba pamoja na kuondosha bomba chakavu. Aidha, wizara kupitia Mamlaka ya Maji itakuwa inatekeleza hatua kwa hatua kwa kadri ya uwezo wa upatikanaji wa fedha za ununuzi wa vifaa vya maji utakavyoruhusu ili kuweza kuondoa changamoto hiyo.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nimeuliza swali nilimuuliza Mhe. Waziri kwamba analifahamu tatizo la maji au upatikanaji wa maji kwa undani katika jimbo la Micheweni nadhani majibu yake alinieleza analifahamu kwa undani zaidi. Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza kabla sijauliza swali la nyongeza uniruhusu nifanye marekebisho madogo katika yale maeneo ambayo ameyataja.

Mhe. Naibu Spika, katika jimbo la Micheweni ninazo shehia saba ambapo miongoni mwa shehia zile tano alizozitaja yeye Shehia ya Mjini Wingwi haimo katika jimbo la Micheweni. Lakini vile vile nataka nimkumbushe tu kwamba, shehia zilizomo ndani ya jimbo la Micheweni ni Shumba Mjini, Majenzi, Micheweni, Chamboni, Kiuyu Mbuyuni, Shaanake na Maziwangómbe. Hizo ndizo ambazo zimeunda jimbo la Micheweni. Kwa hivyo, Shehia ya Mjini Wingwi haiko ndani ya jimbo la Micheweni.

Vile vile, nilitaka kujua kwamba Mhe. Waziri amesema kuwa maeneo yote katika jimbo la Micheweni hayo matano aliyoyasema yeye yanapata maji, lakini nimeweza kuyapunguza na nimeonesha. Kwa kweli, nataka niseme tu kwamba, tumejaribu kufanya utafiti na tunaishi huko kwa hivyo, nataka nimkumbushe baadhi ya maeneo ambayo hayapati maji. Kwa mfano, ukija Micheweni - Chamboni kuna Jichwagumu hawapati maji na hakuna laini ya maji, Msikiti Makumba, kuna Bwawani Chamboni, Kijongwani kuelekea Chumba Mjini, Maziwangómbe kuna Kitonga, Mbuyugowe na maeneo mengine Mtongwe na mengine ndani ya jimbo la Micheweni, ikiwemo hata eneo analoishi Mhe. Mwakilishi kwa maeneo ya pale Chaleni. Haya ni maeneo ambayo ukienda utakuta kwamba shida hiyo ipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa ruhusa yako sasa nimuulize maswali madogo ya nyongeza. Mheshimiwa amesema kwamba moja katika jitihada ni kuwa katika maeneo yale yenye upungufu wa maji juhudi za serikali zitaendelea kufanyika pale fedha zitakapopatikana, nimuombe tu Mhe. Waziri anisaidie kuwaambia wananchi wa Jimbo la Micheweni kwa kuwa jitihada za serikali…

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, uliza swali umekuwa na maelezo marefu mno.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Ni lini hasa mpango huu kwa *target* iliyokusudiwa kwamba uweze kuanza kutekelezwa ili kuona ahadi hii inaweza kutekelezwa kama vile ambavyo itakuwa sawa.

Lakini vile vile niulize swali jengine la pili kwamba kuna Ilani ya CCM…

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, swali la kwanza sikulisikia.

**Mhe. Naibu Spika:** Mhe. Mjumbe, unapouliza swali jaribu kuuliza kwa ufupi sana, ili Mhe. Waziri akuelewe. Wewe unafahamu mwenyewe uliwahi kuwa Naibu Waziri na ulikuwa ukijibu maswali, kadiri swali linapokuwa refu ndio kadiri Mhe. Waziri anashindwa kukupata vizuri.

**Mhe. Shamata Shaame Khamis:** Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee kwa sababu nimeomba ruhusa uniruhusu nitoe maelezo mafupi, lakini nilitaka kujua katika mpango ule ambao Ilani ya CCM imesema kwamba itakuwa na mkakati wa uvunaji wa maji ya mvua, ili kusaidia katika jitihada za upatikanaji wa maji. Mpango huu kwenye ilani umetajwa ni lini utatekelezwa ili kusaidia upatikanaji wa huduma za maji.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kama nimelipata vizuri swali lake linahusu mpango wa uvunaji wa maji ya mvua. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Serikali inayo mpango wa kuandaa utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Taratibu hizo zinaendelea kwa tafiti na itakapokamilika tutatoa taarifa rasmi ya hatua iliyofikiwa na namna ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Mheshimiwa tatizo kama hili la maji lipo katika mji wa Chake Chake Shehia ya Chanjaani, kwa vile shehia ile kisima tunacho ni cha kipindi kirefu.

(a) Je, ni lini sasa Mhe. Waziri wizara yake itatupatia maji kupitia kisima kile.

(b) Je, huu mji wa Chake Chake miongoni mwa matatizo yanayoukumba kuwa maji ni shida ni uchakavu wa hayo mabomba na sisi sio wafaidika wa dola 92 milioni. Je, ni lini sasa kadhia hii ndani ya mji wa Chake Chake ambako ni kimbilio la wafanyakazi pamoja na wafanyabiashara wengi, kadhia hii itatuondokea. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kwanza naomba nimshukuru swahiba wangu kwa maswali yake mazuri.

(a) Mhe. Naibu Spika, nikiri kwamba kuna tatizo katika kisima cha Chanjaani ambacho kwa sasa hakina *pump* ya kusukumia maji. Mhe. Naibu Spika, naomba nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba katika kipindi kifupi kijacho tuna mpango wa kuweka mashine mpya katika kisima cha Chanjaani kuondoa tatizo hili la maji.

(b) Aidha, katika Mji huo Mkuu wa Chake Chake ambako kuna wafanyabiashara wengi na uchakavu wa mabomba naomba pia nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba, kupitia Mradi wa India wa Dola 35 milioni utafika katika maeneo yote ambayo hayakuguswa na mradi ule wa Dola 92 milioni. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Azza Januar Joseph:** Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na nimpe pole kwa kazi hii ngumu kwani maji ni tatizo kubwa linalowasumbua wananchi wengi. Ila naomba tu nimuulize Mhe. Waziri kwamba kuna tatizo limejitokeza kwa wananchi wanaoishi maeneo ya Gombani ilipopita barabara ya Makamu wa Pili wa Rais. Wanananchi hao walikuwa wakipata

maji vizuri sana lakini tokea kutengenezwa kwa barabara ile hadi leo wananchi wale wanahangaika kupata maji, hawapati maji hata kidogo.

Je, ni lini wizara itafanya marekebisho ili waweze kurudishiwa huduma hii ya maji.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, nimeanza kulifuatilia suala hili ambalo Mhe. Mwakilishi amelieleza na hatua za utekelezaji wa kurejesha huduma katika eneo hilo zinaendelea, katika muda mfupi ujao huduma itaanza kupatikana. Naomba kuwasilisha mheshimiwa.

**Mhe. Naibu Spika:**Nataka nitoe *offer, very special offer* kwa Mhe. Zaina Abdalla Salum.

**Mhe. Zaina Abdalla Salum:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa *offer* hii ya asubuhi ya leo. Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri nimpongeze sana kwa majibu yake ya maswali yote yaliyoulizwa. Lakini Mhe. Waziri nataka nimwambie kwamba katika changamoto hii ya maji basi pia jimbo la Bububu nalo limekumbwa na changamoto hii katika maeneo mengi kama vile ya Mbuzini, Mkanyageni, Kidichi na maeneo mengine.

Je, Mhe. Waziri katika utafiri wake alioufanya atahakikisha vipi kuwa jimbo la Bububu katika maeneo hayo niliyoyataja kuwa yanaweza yakapatiwa maji kwa ufasaha. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Maji, Nishati na Madini:** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kuhusiana na maeneo ambayo hayapati maji au yana upungufu mkubwa wa maji katika jimbo la Bububu.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Mwakilishi kwa pamoja mimi na yeye tutembelee maeneo yote ambayo yana upungufu wa maji ili tuone tunatatua vipi changamoto hiyo ya upungufu wa maji katika eneo hilo.

**Nam. 25**

**Kuzifanyia Matengenezo Barabara za Miwani, Mwera na Fuoni**

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Kny: Mhe. Salma Mussa Bilal)** - Aliuliza:-

Naipongeza kwa dhati serikali kwa juhudi zake ambazo inazichukua katika kuzifanyia matengenezo barabara zetu.

Ni lini serikali itazifanyia matengenezo barabara za Miwani, Mwera na Fuoni Kwachimbeni, ili kuwaondolea usumbufu wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, barabara ya Kizimbani, Miwani hadi Kiboje (km 7.2) ni miongoni mwa barabara zilizotajwa kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2020-2025 ya kuendeleza ujenzi wa barabara hiyo kwa kujengwa kiwango cha lami. Aidha, kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021 serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.0 kwa ajili ya kuanza mradi wa ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Wizara kupitia Wakala wa Barabara Zanzibar imeanza maandalizi ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kusafisha eneo la barabara urefu wa kilomita 1.0 kuanzia Mndo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa matengenezo ya barabara ya Mwera hadi Fuoni Kwachimbeni, serikali inatambua umuhimu wa barabara hiyo na tayari imo kwenye Mpango Kazi wa miaka mitano 2021-2025 kuijenga kwa kiwango cha lami. Aidha, serikali itakuwa ikiifanyia matengenezo sehemu zote mbaya kwenye barabara hiyo ili iweze kupitika wakati wote kwa urahisi. Ahsante nashukuru Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Yussuf Hassan Iddi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri napenda kuuliza swali la nyongeza lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa wananchi wa Kizimbani, Miwani na Kiboje wana hamu sana na barabara yao hii kukamilika. Je, ni lini serikali itajitahidi kukamilisha barabara hiyo ili wananchi wapate kuitumia.

(b) Kwa kuwa barabara ya Mwera hadi Fuoni Meli Saba Kwachimbeni wamesema imo kwenye mpango wa mwaka 2021 - 2025, lakini kwa kuwa barabara hiyo iko katika hali mbaya na haipitiki hivi sasa. Ni lini serikali itafanya matengenezo ya dharura kwa ajili ya barabara hiyo. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu swali la nyongeza Mhe. Mwakilishi lenye kitoto (a) na (b) kama ifuatavyo.

Swali langu la msingi nilikuwa nimeshasema kwamba tayari tumetenga fedha shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kuitengeneza barabara ya Kizimbani – Kiboje. Tunatambua kweli ile barabara ni mbovu lakini kama tulivyosema kwanza barabara zinakuwa zinatumia gharama kubwa na mimi mwenyewe nimekwenda nimeiona kweli ni mbovu sana, lakini tumo katika jitihada ya kuitengeneza hiyo barabara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Issa Haji Ussi:** Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi na kabla ya kuuliza swali langu kwa Mhe. Waziri nilikuwa nina nukta moja tu nataka niseme, nayo ni kuomba tu. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wa Chwaka tuwaombee kila la kheri Klabu ya Simba leo ifanye vizuri, wao ni wawakilishi pekee katika *Champion League* kwa upande wa Tanzania, tuwaombee kheri na baraka tunatambua uwezo wa Al-Ahli ni mkubwa, lakini Mwenyezi Mungu atakuwa pamoja nasi Watanzania tutafanya vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Baada ya maelezo hayo sasa niombe ruhusa yako kuuliza swali moja kwa Mhe. Waziri. Pamoja na jitihada nzuri za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwaletea maendeleo wananchi wake zikiwemo huduma zote za msingi pamoja na huduma za kijamii. Serikali imefanya jitihada kubwa katika miundombinu ya barabara na hasa kwa vijijini katika Mradi wa *MIVARF*. Barabara hizi chini ya Mradi wa *MIVARF* malengo yake makubwa ilikuwa ni kuimarisha upatikanaji wa mazao ili kurahisisha usafirishaji wa mazao hayo kufika sokoni.

Je, serikali ina mpango gani wa kuziimarisha barabara za *MIVARF* ambazo lengo lake ni kuimarisha upatikanaji wa mazao kwa watu mijini na kuimarisha uzalishaji wa mazao kutoka vijijini kutokana na hali ya uchakavu mkubwa katika barabara hizi. Kwa mfano, barabara zilioko Ndijani, Makunduchi, Mtule, Kiboje, Miwani, maeneo yote haya yalikuwa yamewekezwa fedha nyingi za serikali na barabara hizi zimekuwa hazipitiki. Je, serikali ina mpango gani wa msingi katika kuziimarisha barabara hizi, ili kuhuisha malengo yaliyokusudiwa katika ujenzi wa barabara hizi.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa upande wa matengenezo ya barabara serikali inatambua barabara zote haichagui hii ya *MIVARF* hii ya sehemu gani. Kwa hivyo, barabara zote zitajengwa kwa mujibu wa mpango kazi ambao upo, lakini haitochagua kwamba hii imetengenezwa na *MIVARF* hii imetengenezwa na nani, barabara zote sisi tunajua ni muhimu na zote tutazitengeneza kwa mujibu wa uwezo ambao uliokuwepo. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

**Nam. 74**

**Utiaji wa Matuta na Alama za Barabarani *(Road Signs)* Barabara ya Ole – Kengeja**

**Mhe. Bakar Hamad Bakar** - Aliuliza:-

Rais wa Awamu ya Saba Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein aliifungua barabara ya Ole - Kengeja katika mwezi wa Oktoba, 2020. Katika ufunguzi huo aliwataka wasimamizi wa barabara kuharakisha utiaji wa matuta pamoja na alama za barabarani (*road signs*), ili kuepusha ajali ambazo zingeweza kujitokeza kwa kutokuwepo kwa vitu hivyo.

(a) Je, ni lini serikali inatarajia kukamilisha uwekaji wa matuta na alama za barabarani katika barabara Ole - Kengeja.

(b) Je, ni hatua gani ilizofikia katika ujenzi wa kipande cha barabara kilichobakia kutoka Kengeja hadi Mtambile na ni lini inatarajiwa kukamilika.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi -** Alijibu:-

Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, wizara yangu tayari imeshaomba fedha kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kuikamilisha kazi iliyobakia ikiwemo kazi ya kuweka matuta na alama za barabarani katika barabara ya Ole- Kengeja.

b) Mhe. Naibu Spika, serikali inatarajia kumalizia kipande hiki kutoka Kengeja hadi Mtambile katika bajeti ya mwaka 2021 – 2022 chini ya Mfuko wa Barabara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Bakar Hamad Bakar:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa majibu yake mazuri aliyonijibu kwenye swali langu hilo. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa kwenye ujenzi wa barabara ile kuna vipando vya wananchi viliharibiwa minazi, miembe na vitu vyengine mbali mbali. Je, ni lini serikali itawalipa wananchi wale na ni kiasi gani kimetengwa kuwalipa wananchi hao. Ahsante.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Bakar Hamad Bakar swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Suala la fidia kwa upande wa wizara lina changamoto kubwa sana kwa sababu, wananchi huwa wanafanyiwa tathmini kabla ya kujengwa barabara na unapata idadi gani jumla ya fedha za kuwalipa wale wananchi, lakini baada ya kujengwa kwa barabara pia hwa inatokezea changamoto za madai. Kwa hivyo, ile fedha ya kuwalipa huwa inakuwa inaongezeka lakini kwa sasa tumeandaa utaratibu mzuri wa kuwalipa fidia wananchi na tunazifanyia *review* zote fidia ambazo zipo zikiwemo za Ole- Kengeja. Kwa sasa tayari tumekaa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, ili kufanya *review* kuweka utaratibu mzuri wa kulipa fidia na sio wa Ole-Kengeja tu kwa sababu fidia hazipo Ole- Kengeja hata katika maeneo mengine. Kwa hivyo, tunatengeneza utaratibu mzuri ili kulipa fidia ambazo zipo.

**Mhe. Shaib Hassan Kaduara:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba basi nimuulize swali la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

(a) Mhe. Waziri, sijui atakubaliana na mimi kwamba wizara yake ina tabia ya makusudi ya kwamba haikamilishi kazi zake maeneo husika. Kwa mfano, ni juzi tu walifanya kazi ya uzibaji viraka maeneo ya barabara ya Mkoani wakaishia Chanjamjawiri na hapo wakaacha baadhi ya maeneo Matuleni. Je, suala hili atalisimamiaje waziri.

(b) Kuna baadhi ya maeneo ukitoka Chanjaani- Pujini vile vile kuna tatizo kama hilo. Je, Mhe. Waziri suala hili ataliondosha vipi.

**Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyogeza Mhe. Shaib Hassan Kaduara kama ifuatavyo. Katika zoezi la uzibaji viraka ni zoezi endelevu ambalo tumeanza Unguja na Pemba kidogo. Kwa hivyo, inategemea na lami tuliyokuwa tunayo, tukipata lami tutakuwa tunaendelea. Kwa sababu lengo letu ni kuziba viraka vyote ambavyo vipo Zanzibar hatutaki kuwa na mashimo,

hata sisi mashimo yanatukera sana. Kwa hivyo, viraka tutaviziba kwa kadri ya lami itakavyopatikana

**Mhe. Naibu Spika:** Ahsante Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umemalizika, ingawa nitaongeza dakika 15 ili tuweze kumaliza maswali tuliyokuwa nayo lakini hata hivyo kwa sababu tuna taarifa ambazo hazituhitaji kujadiliwa. Kwa hivyo, tutakuwa na muda wa kutosha wa kuweza kumaliza siku ya leo na shughuli zetu ambazo tumejipangia, kwa hivyo naomba sasa Mhe. Hassan Hamad Omar kwa ajili ya swali Nam 38. Mwakilishi wa Jimbo la Kojani. Mhe. Hassan Hamad Omar hayupo.

**Nam. 38**

**Hatua Zilizofikiwa katika Kutumia Bahari kwa Maendeleo Endelevu Zanzibar**

**Mhe. Habib Ali Mohamed (Kny. Mhe. Hassan Hamad Omar) –** Aliuliza:-

Katika Malengo ya Maendeleo Endelevu Namba. 14 imeelezwa kuwa shughuli za uvuvi iwe moja kwa moja au vyenginevyo, huajiri watu wengi. Kwa hiyo, Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi imeanzisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, ili kuhifadhi na kutumia bahari kwa maendeleo endelevu.

(a) Je, Kampuni ya Uvuvi iliyoanzishwa kipindi cha Dkt. Ali Mohamed Shein na kuahidiwa makubwa imesaidia nini kwa wananchi na serikali kwa ujumla.

(b) Je, meli nne za uvuvi wa bahari kuu zinazotarajiwa kuletwa Zanzibar kutoka Tanzania Bara zitasaidia vipi kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma za biashara ya samaki kwa wachuuzi na walaji wanyonge.

(c) Je, inatarajiwa kuajiri watu wangapi kwa kila meli.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 38 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Kampuni ya Uvuvi ya *ZAFICO* imesaidia wananchi wadogo wadogo na wananchi wengine wa Zanzibar upatikanaji wa samaki wanaovuliwa kwa boti yake ya Sehewa II na kuuzwa kwa mnada katika diko la muda la Msikiti Mabuluu. Mhe. Naibu Spika, *ZAFICO* pia imefanya mafunzo mbali mbali kwa wananchi wanaojishughulisha na biashara ya dagaa wakiwemo, wamiliki wa boti, wavuvi, manahodha na wasarifu wa dagaa. Mafunzo hayo yaliwahusisha wananchi katika madiko ya Maruhubi, Mangapwani na Fungurefu - Mkokotoni. Mafunzo hayo pia yanatarijiwa kufanyika katika maeneo mengine ya Unguja na Pemba.

Hata hivyo, *ZAFICO* ina mpango wa kutekeleza miradi mitatu ikiwemo Mradi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa Fungurefu Mkokotoni, Kiwanda cha Kusarifu Minofu ya Samaki na Mradi wa Ufugaji wa Samaki Baharini. Hivyo, miradi hiyo inatarajia kutoa ajira kwa wananchi wa Zanzibar.

(b) Mhe. Naibu Spika, meli nne za uvuvi za bahari kuu zinazotarajiwa kuja Zanzibar ni kupitia mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo *(IFAD).* Hivyo, meli hizo zitaongeza upatikanaji wa samaki kwa wingi katika masoko ya samaki na kukuza biashara ya samaki kwa wachuuzi wa Zanzibar.

(c) Mhe. Naibu Spika, meli nne za uvuvi zinazotaraijiwa kuja Zanzibar zinategemewa kuajiri jumla ya wafanyakazi wasiopungua 8 kwa kila meli moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Ameir Abdallah Ameir:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii naomba niulize swali moja la nyongeza. Lakini kabla sijauliza naomba nitoe maelezo mafupi sana, naomba nim-*quote* Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein wa awamu iliyopita Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa soko la kisasa kwa ajili ya wavuvi liliopo Malindi Zanzibar alisema maneno haya “Zanzibar inayo hazina ya rasilimali za baharini ikiwemo samaki wakubwa ambao wakivuliwa wataongeza pato la wavuvi”. Lakini vile vile, kwa utafiti mdogo ambao umefanywa na Chuo Kikuu cha Wengen kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirikiano Ujerumani 2017 walisema kwamba wavuvi wa Zanzibar wadogo wadogo wanazalisha tani 14 hadi tani 20 elfu kwa mwaka kwa ajili ya mahitaji madogo madogo ya kifamilia. Swali langu lipo hapa.

(a) Je, wizara ina mkakati gani ya kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo kuweza sasa kuvua samaki wakubwa kwa kutumia vyombo ambavyo ni vya kisasa na kuacha kutumia vyombo ambavyo vipo katika hali duni kabisa.

(b) Je, wizara ina jiandaa vipi kukabiliana na suala zima la uvuvi haramu kuelekea katika kuimarisha Uchumi wetu wa Buluu. Ahsante sana.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa maswali mazuri sana. Mhe. Naibu Spika, mikakati tuliyonayo kuwasaidia wavuvi wadogo wadogo, nafikiri unaelewa vizuri kwamba karibuni tulisaini mkataba tumeingia na wawekezaji watakaojenga bandari ya kisasa pale Mpigaduri. Moja katika chelezo zitakazo jengwa ni kutengeneza boti na zana za uvuvi zitakazo wasaidia wavuvi wadogo wadogo. Kwa hivyo, huo ni mkakati mmoja lakini vile vile, kuna wawekezaji tayari wamefika Zanzibar wanataka kuingia mikataba na wananchi, wavuvi wadogo wadogo, ili waweze kuvua katika hiyo misingi unayoieleza kuweza kushirikiana baina ya hawa wavuvi wadogo wadogo pamoja na wawekezaji. Mhe. Mjumbe, swali la pili.

**Mhe. Naibu Spika:** Lilikuwa na (a) na (b).

**Mhe. Ameir Abdallah Ameir:** Ahsante Mhe. Naibu Spika, swali la mikakati ya uvuvi haramu. Wizara inajiandaaje kukabiliana na suala la uvuvi haramu.

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi**: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kwamba tayari wizara imeunda Idara Maalum ya *Conservation*, ambayo kazi yake ni kupitia maeneo yote ambayo tumeyahifadhi, vile vile kuhakikisha kwamba uvuvi wote unaofanywa ni uvuvi ambao umeruhusiwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hivyo, tayari wizara inayo idara inyosimamia suala la uvuvi haramu.

**Nam. 48**

**Mikakati ya Serikali Kuweka Utaratibu wa Kukabiliana na Matatizo ya Udhalilishaji katika Jamii**

**Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa -** Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwa na sheria na mikakati ya kukabiliana na udhalilishaji wa akinamama na watoto. Moja ya mikakati hiyo ni kuwaweka waratibu wa kukabiliana na wimbi la udhalilishaji katika ngazi za shehia na wilaya.

(a) Je, kuna waratibu wangapi katika Mkoa wa Mjini Magharibi.

(b) Je, serikali inatoa posho kiasi gani kwa kila mratibu kwa mwezi.

(c) Je kuna utaratibu wowote kuwafuatilia na kuweza kujua changamoto zinazowakabili.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto) -** Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwanza tumepokea pongezi hizo za Mhe. Mwakilishi kwa kutambua juhudi na mikakati inayochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuondoa tatizo la vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia nchini. Mhe. Naibu Spika, Mkoa wa Mjini Magharibi una jumla ya Waratibu wa Wanawake na Watoto 122 ambao wamegawanya katika shehia zote za mkoa huo kama ifuatavyo. Wilaya ya Mjini ina waratibu 56, Wilaya ya Magharibi “A” ina waratibu 34 na Magharibi “B” ina waratibu 32.

(b) Mhe. Naibu Spika, serikali inawapatia posho la usafiri la shilingi 10,000/- hadi 20,000/= kwa ajili ya ufatiliaji wa wahanga wa matukio kwa kila wilaya kwa awamu, mgao huu unategemea jinsi fedha zinavyopatikana. Aidha, pamoja na wizara kuweka kiwango hicho pia Shirika la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* Kanda ya Zanzibar limekuwa likitoa posho kama hizo kwa waratibu katika Mkoa

wa Mjini na mikoa mengine Unguja na Pemba kwa lengo la kuwawezesha kuwafikia wahanga wa matukio hayo, ili kuwasaidia kupatikana kwa taarifa za matukio.

(c) Mhe. Spika, wizara imeweka utaratibu maalum wa kufuatilia na kujua changamoto zinazowakabili waratibu hadi ngazi za shehia katika kila wilaya. Waratibu hufanya vikao vya kila mwezi ambapo lengo ni kupeana miongozo ya utendaji na kubadilishana na uzoefu katika utendaji kwa kuongeza kiwango cha ufanisi katika shughuli zao za kujitolea za kila siku. Aidha, Afisa wa Wanawake na Watoto ngazi ya wilaya ni msimamizi katika kuratibu changamoto zao na kuchukua hatua stahiki kwa kushirikiana na Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoa ili kuona kwamba changamoto zilizopo zinapatiwa ufumbuzi.

**Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nataka kumuuliza swali la nyongeza. Kutokana na hali wanazopambana na udhalilishaji waratibu hao na kwa kuwa umetwambia wanapatiwa posho 10,000/= mpaka 20,000/=.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kuwawezesha waratibu hawa kujikimu na hali ya maisha.

(b) Je, ndani ya Mkoa wa Mjini wa Magharibi kuna waratibu wangapi

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kny: Mhe. Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa swali lake la nyongeza lenye vitoto (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu mama nimesema kama Mkoa wa Mjini Magharibi una jumla ya Waratibu wa Wanawake na Watoto 122 na wamegawanywa katika shehia zote kama nilivyojibu mwanzo ambavyo Wilaya ya Mjini ina waratibu 56, wilaya ya Magharibi “B” 32 na Wilaya ya Magharibi “A” 34.

b) Swali lake la kuhusiana na suala la kujikimu kwa hali ya maisha Mhe. Naibu Spika, sisi kwa upande wa serikali tunatambua umuhimu wa waratibu hawa kwa kazi wanayoifanya pamoja na wadau wote katika kupambana na suala zima la udhalilishaji. Sisi tunaangalia kutokana na hali yetu ya kifedha kama wizara na kila hali itakaporuhusu basi tutaangalia kwa sababu suala hili ni mtambuka linagusa katika maeneo tofauti. Kwa hivyo, nimuahidi kwamba sisi kwa upande wa wizara tutachukua mawazo yake na fikra zake katika kulipa umuhimu suala la udhalilishaji kama ambavyo Mhe. Rais alipoonana na wadau walivyolizungumza. Kwa hiyo tutalifanyia kazi kadri hali itakavyoruhusu katika suala zima la kuwasaidia hawa na kuwawezesha na kwenda sambamba na hali zao za kimaisha. Ahsante sana.

**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman:** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kuniona na kunipatia nafasi ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo. Lakini Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumuuliza Mhe. Waziri swali naomba kwanza na mimi nichukue fursa hii kuwatakia kila la kheri Simba *Sports Club*. *(Makofi)*

(a) Mhe. Waziri wakati akijibu jibu lake alisema, Mhe. Naibu Spika, serikali inawapatia posho la usafiri wa shilingi 10,000/- hadi 20,000/- waratibu hao. Naomba kujua ni utaratibu gani unaotumika na kujiridhisha kwamba ile fedha inawafika walengwa hawa.

(b) Mhe. Waziri yuko tayari kufuatana na mimi kwena kuwasikiliza changamoto na matatizo ya waratibu hao. Ahsante sana Mheshimiwa.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Shadya Mohamed Suleiman swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, serikali hufanya malipo kwa njia mbili au katika njia ambayo inayotumika hasa ni kwa ajili ya kulipa fedha zao kwa mujibu wa *account* za watumishi wa umma. Lakini pale ambapo panapokuwa panahitajika fedha kwa ajili ya matumizi au kutokana na hali kwamba wahusika hawana *bank account* hasa katika suala hili zima la uratibu, basi tuna utaratibu wa kiserikali kutokana na mazingira yalivyo, eneo husika tunaangalia jiografiya ilivyo halafu tunahakikisha zile fedha zinafika kwa kushirikiana pamoja na halmashauri zetu, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa na Masheha. Kwa hiyo katika suala hilo nimtoe wasiwasi Mhe. Mwakilishi wala asiwe na hofu.

(b) Swali la kuwa niko tayari katika kufuatana na yeye, katika kuhakikisha kwamba kupambana na hili kwa ujumla. Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme kwamba yeye alikuwa Mhe. Naibu Waziri ana uzoefu katika hili. Sisi kwa upande wa serikali tunathamini ushauri wa kila mmoja, kwa hiyo sisi kwa upande wetu na mimi kwa upande wa wafanyakazi na watumishi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto hatutosita kupokea ushauri na wala sio kwake yeye tu, isipokuwa kwa mtu yeyote ambapo hasa tumeelekezwa na Mhe. Rais, kwa hivyo mimi nitakuwa tayari pamoja na yeye kushirikiana pamoja na watendaji na wawakilishi wote wengine. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Nam. 62**

**Kuchelewa Ujenzi wa Hospitali ya Wete**

**Mhe. Habib Ali Mohamed** - Aliuliza:-

Jamii ya Wazanzibari inakabiliwa na maradhi tofauti yanayoathiri afya na kusababisha vifo ambapo watu wengi wanalalamika wa ndani na nje ya nchi na kuamua kutoa michango mbali mbali.

a) Je, kuna sababu zipi zilizopelekea kusitisha ujenzi wa hospitali ya kisasa Wete.

b) Je, serikali imeweka mikakati gani ya kukabiliana na maradhi sugu kama vile, sukari, *pressure*, *cancer*, mifupa na kiharusi.

c) Je, serikali ina mkakati gani juu ya kuwapatia matibabu watu walioathirika na vurugu za baada ya uchaguzi wa 2020.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto)** - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 62 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, mradi wa ujenzi wa hospitali ya kisasa ya Wete ni moja kati ya vipaumbele vya iliyokuwa Wizara ya Afya hapo kabla na pia ni moja ya mkakati katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba mradi huu haujasitishwa bali upo katika hatua za awali za utekelezaji wake. Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Abudhabi tayari imeunda Kitengo cha Usimamizi wa Mradi *“Project Implementation Unit – PIU”* kwa lengo la kupata ufanisi katika utekelezaji wake.

Mhe. Naibu Spika, mradi huu unatarajiwa kuhusisha ujenzi wa majengo mapya, ukarabati na upanuzi kwa baadhi ya majengo. Mkataba tayari umeshasainiwa na serikali hizi mbili (Abudhabi na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar) na ujenzi unatarajiwa kuanza mwaka wa fedha 2021/2022. Mradi huo unagharamiwa na Serikali ya Abudhabi, ambapo shilingi bilioni 23 tayari zimetengwa na serikali hiyo kwa ajili ya kufanikisha azma hii.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia mabadiliko ya viongozi katika taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, wizara itafuatilia hatua kwa hatua utekelezaji wa mradi huo. Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa mikakati inayotekelezwa ni kuwapatia elimu ya maradhi yasiyoambukiza watungaji wa sera ili kuandaa sera zenye mwelekeo wa kuzua au kupunguza maradhi yasiyoambukiza.

Vile vile, kuhakikisha kwamba viongozi kuanzia ngazi za chini hadi uongozi wa juu wa serikali wanalizungumzia suala zima la maradhi haya katika vikao mbali mbali na kuunga mkono juhudi za serikali za kupambana na kudhibiti ongezeko la maradhi yasiyoambukiza. Aidha, kutoa elimu kwa jamii juu ya kujikinga, kugundua mapema na kupata tiba sahihi ya maradhi hayo kupitia mikutano, vyombo vya habari na usambazaji wa vipeperushi. Lengo ni kuifanya jamii ipate uelewa na kubadilisha mfumo wa maisha unaochangia kuongezeka maradhi haya.

Mhe. Naibu Spika, wizara imeongeza upatikanaji wa huduma za maradhi yasiyoambukiza kutoka vituo nane vilivyokuwepo mwaka 2012 hadi kufikia jumla ya vituo 53 mwaka 2020 kwa Unguja na Pemba. Pia, mafunzo yanaendelea kutolea kwa watendaji wanaotoa huduma katika hospitali na vituo vya Afya kwa mujibu wa muongozo wa matibabu wa maradhi hayo kwa dhamira nzima ya kutoa huduma zilizo bora.

Aidha, wizara imeimarisha mfumo wa upatikanaji wa taarifa za maradhi hayo kwa kuweka daftari la kumbukumbu za wagonjwa wanaofika vituoni, ili kujua hali halisi ya maradhi haya, sambamba na ufanyaji wa tafiti mbali mbali ili kujua ukubwa wa tatizo na hatimae kuweza kupanga mikakati ya kudhibiti na kupunguza ongezeko la maradhi haya sugu au yasiyoambukiza.

Mhe. Naibu Spika, Sera ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kutoa huduma za afya kinga na tiba bure kwa wananchi wote bila ya ubaguzi wa rangi au sehemu anayotoka. Kwa mustakbal huo, wananchi wote wenye matatizo ya kiafya wanatakiwa kufika katika hospitali na vituo vya afya, ili kupatiwa huduma za matibabu. Hivyo, katika kipindi hicho cha uchaguzi wale wote waliopata matatizo na kufika katika hospitali walipatiwa huduma. Ikiwa kama kuna watu ambao walipata majeraha na hadi sasa hawajapata huduma, wizara inawataka kufika katika vituo vya afya kwa kupatiwa matibabu. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Hili swali lina (a) (b) na (c) Mheshimiwa umefikia kwenye (b) naomba undele na (c) Umejibu (c) pia. Huku kwangu liko tofauti mheshimiwa. Tunaendela swali la mwanzo la nyongeza.

**Mhe. Habib Ali Mohamed:** Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Namshukuru kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa ni kipindi kirefu sasa hivi kisichopungua miezi 6, mashine ya *CT-Scan* katika Hospitali ya Abdalla Mzee kisiwani Pemba haifanyi kazi na wagonjwa hao sasa hivi wanapata huduma hiyo katika kisiwa cha Unguja. Je serikali inachukua hatua gani za kuhakikisha kama mashine ile inafanyiwa matengenezo au kununuliwa mashine mpya ambayo itawahudumikia wakaazi wa Kisiwa cha Pemba. Ahsante.

**Mhe.Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, suala la *CT-Scan* juu ya Hospitali ya Abdalla Mzee tunalifahamu na tumekuwa tunapata changamoto mwanzo kutokana na hali ya umeme katika kipindi cha nyuma. Katika vifaa ambavyo tunataka tuhakikishe kama vinafanya kazi, tunaendanalo kwa kasi na nimuombe tu Mhe. Mwakilishi aendelee kuwa mvumilivu. Tunatambua kwamba mashine ile ni muhimu na huduma hii ni muhimu kwa ajili ya wananchi sio tu kwa ajili ya Pemba lakini umuhimu kwa ujumla ni kwamba uwepo katika kuhakikisha kwamba wale wanaokwenda wanapata kile wanachostahiki. Kwa hiyo, tutazidi kulifuatilia na nimuhakikishie kwamba tutalifanyia kazi kwa juhudi ya ziada. Ahsante sana.

**Mhe. Maryam Thani Juma:** Ahante Mhe. Naibu Spika kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Waziri kwenye jibu lake mama alisema huu mpango wa ujenzi wa Hospitali ya Wete upo katika hatua za awali za utekelezaji wake. Je nilikuwa nataka nijue ni hatua gani za awali zilizochukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, alisema kwamba wanajitahidi kukabiliana na maradhi ambayo wameyataja kwenye jibu lake mama lakini tukiangalia tunajenga hospitali ya kisasa na katika hospitali hii ina upungufu sana ya vifaa tiba ikiwemo X-*Ray*, *ultrasound* na mambo mengine. Je anatuhakikishiaje baada ya ujenzi huu, vifaa hivi vitakuwepo vya kutosha na vitawapunguzia usumbufu wananchi wanaotumia hospitali ile.

**Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali (Kaimu Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto):** Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Maryam Thani Juma swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, katika majibu yangu mwanzo nilisema kwamba *project* hii sasa hivi ipo katika *initial project* ambapo tumeunda kitengo cha *PIU* yaani *Project Impelementation Unit* na tunaendelea kufuatilia kutokana na hatua itakayokuwepo. Inawezekana kwamba kutokana na mabadiliko ya awamu iliyopita pia na awamu hii yetu ya nane kwamba tunakuwa na mikakati tofuati kuzidi kuangalia na kufanya utafiti wa kina zaidi katika mahitaji ambayo tunataka tuyaboreshe.

Kwa hiyo, ujenzi wa hospitali upo pale pale na serikali imekusudia kwa sababu ya umuhimu wake kutokana na mahitaji ya wananchi tunayokwenda nayo. Changamoto tulizokuwa nazo ni kubwa hasa katika maeneo ya sekta ya afya, hasa katika kuhakikisha kwamba huduma hizi wanazozihitaji wananchi zinakwenda katika maeneo yote wanayostahiki.

Kwenye hospitali ya kisasa aliyokusudia yeye, hakutaja hospitali gani lakini kwa ufahamu mimi nimechukulia kwamba ni Hospitali ya Binguni na mradi kama nimemfahamu vizuri. Azma ya kujenga mradi huu ni kubwa, utakuwa una vifaa na maeneo ya kutosha na hivi sasa serikali ipo katika kujinga zaidi kuhakikisha kwamba mradi huu unakwenda kama ulivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, tunayo changamoto kubwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa sababu Mnazi Mmoja ni Hosptali ya Rufaa na ukimbiliaji wa wananchi kufata huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja inakuwa wakati wengine tunazidiwa. Kwa hiyo, kupitia Baraza lako tuwaombe wananchi kwa huduma ambazo wanazihitaji wazidi kuzifuata katika wilaya zao na katika maeneo husika. Kwa mfano sisi kwa upande wa Mnazi Mmoja tuna madaktari bingwa 42, *general practitioners 102*, wauguzi 560 na maabara 74.

Mhe. Naibu Spika, halikadhalika tunazo changamoto katika madaktari hawa. Ndio maana sasa serikali kupitia Chuo cha Afya sasa hivi tunaendesha *course* tofauti kama sasa hivi tuna *course* ya kusomesha masuala ya meno, (*School of Dentistry)*, ili tuna madaktari wetu baada ya muda na wale ambao wanasoma nje watakuja kusaidia katika kutoa huduma hizi katika hizi hospitali kubwa, ambazo tayari tunayo miradi ya kujenga, tuhakikishe kwamba tunajenga lakini pia tunakuwa tuna wafanyakazi wa kutosha katika kutoa huduma. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

**Mhe. Naibu Spika:** Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali umemalizika. Niliongeza tena dakika 15 lakini pia zimezidi zaidi ya dakika 15. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa usikivu na utulivu wenu. Bado tunaendelea na utaratibu mwengine ambao nitamuachia Mhe. Mwenyekiti Shaaban Ali Othman aje aendelee na shughuli zinazofuata. Mhe. Mwenyekiti karibu sana.

(*Hapa Mhe. Mwenyekiti, Shaaban Ali Othman alikalia kiti)*

## KAULI YA SERIKALI

### Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya Mwaka 2020

**Mhe. Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kufika hapa wazima na kutekeleza wajibu wetu huu, lakini pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 383 ya mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya taarifa hii ni kuliarifu Baraza la Wawakilishi ya kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo mwezi wa Mei 2020 limepitisha Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020 (*The Deep Sea Fisheries Management and Development Act, (CAP 388 R.E. 2020)* na kusainiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Joseph Pombe Magufuli mwezi Juni 2020.

Mhe. Mwenyekiti, kulingana na utaratibu wa kifungu cha 1 cha sheria hiyo, imeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 12 Oktoba, 2020 kupitia Tangazo la Serikali Namba. 883 la mwaka 2020 (GN. No. 883 of 2020). Aidha, kwa kukidhi matakwa ya Katiba ya Zanzibar ibara ya 132 (1) na (2) inayoelekeza sheria yoyote itakayopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambayo itatumika Zanzibar, ipelekwe katika Baraza la Wawakilishi na Waziri husika kwa lengo la kuorodheshwa.

Mhe. Mwenyekiti, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga na kupitisha Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Nam. 1 ya 1998 (*The Deep Sea Fishing Authority Act. No. 1. 1998*) na hatimae Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ikaanzisha Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti shughuli za uvuvi katika eneo la Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (yaani *Exclusive Economic Zone - EEZ*). Lengo la kuanzishwa kwa chombo hicho ilikuwa ni kudhibiti na kusimamia kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania shughuli zote za uvuvi katika eneo la Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari wenye urefu wa kiasi cha maili 200 za bahari (200 *nautical miles)* kutoka ufukweni.

Hata hivyo, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ilishindwa kuanza kazi zake hadi mwaka 2010 kutokana na kuwepo changamoto mbali mbali. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:-

- Kutoorodheshwa Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu na Baraza la Wawakilishi kutokana na kukosekana kwa uwakilishi wa pande mbili za Muungano katika menejimenti ya Mamlaka,
- Mgawanyo wa mapato yatokanayo na uvuvi wa bahari kuu, na
- Kukosekana ushirikishwaji wa wadau wa pande zote mbili za Muungano wakati wa maandalizi ya sheria husika.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Sheria ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Nam. 1 ya 1998 ilifanyiwa marekebisho na Sheria Nam 4 ya mwaka 2007 ambapo suala la uwakilishi na mgawanyo wa mapato lilizingatiwa kikamilifu. Pamoja na marekebisho hayo, Sheria ya kuanzisha Mamlaka bado haikuorodheshwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kutoorodheshwa kwa sheria hiyo kumepelekea Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu kuendeshwa katika kipindi cha mpito kwa muda wa miaka 10 na kutoweza kutekeleza majukumu yake ya kisheria kwa ufanisi. Kutokana na hali hiyo na kuondoa changamoto hii, Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu iliandaa Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 (*Deep Sea Fisheries Management and Development Act, CAP 388 R.E. 2020*), iliyoshirikisha wadau wa pande zote mbili za Muungano na kuhakikisha kuwa kero zote zinazohusiana na sheria ya zamani zimejadiliwa na kufikia muwafaka pamoja na kupata ridhaa ya pande zote mbili.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi cha tarehe 3 Februari 2021 iliridhia mapendekezo ya kuwasilishwa kwa Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020 kwa lengo la kuorodheshwa katika Baraza lako tukufu. Kiujumla sheria hii mpya imekuwa shirikishi na kigezo kwa Sheria nyengine zisizo za Muungano ambazo zinatumika katika pande mbili za Jamhuri ya Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi si miongoni mwa masuala ya muungano kwa mujibu wa Ibara ya 4(3) na Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1978. Hata hivyo, uvuvi katika Ukanda Maalum wa Uchumi wa Bahari (*EEZ*) unasimamiwa na Sheria mpya ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020, ambayo inahusisha pande mbili za Jamhuri ya Muungano na utaratibu wa utekelezaji wake lazima uzingatie matakwa ya kikatiba.

Hivyo, ili kukidhi matakwa ya Katiba ya Zanzibar ibara ya 132 (1) na (2) ni lazima sheria hiyo ipitishwe katika Baraza la Wawakilishi na Waziri husika kwa lengo la kuorodheshwa. Kwa mantiki hiyo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inawasilisha Waraka kuhusu Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura ya 388 ya mwaka 2020, kwa ajili ya kupata baraka za Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuorodheshwa katika sheria zinazotambulika na Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020 ina sehemu kumi na nne (14) ambazo kwa muhtasari zimejumuisha mambo yafuatayo:

Sehemu ya Kwanza, inahusisha vifungu vya utangulizi ikijumuisha Jina fupi la Sheria, kuanza kutumika kwa Sheria, tafsiri ya maneno yaliyotumika na mawanda ya sheria.

Sehemu ya Pili, imebainisha kuanzishwa kwa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu na kazi zake.

Sehemu ya Tatu, inaainisha uongozi wa Mamlaka ikiwemo muundo wa Mamlaka, Kamati Tendaji na kazi zake, Kamati ya Ushauri na Kazi zake, Menejimenti ya Mamlaka, uteuzi na sifa yaani "*qualifications"* za uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu na Naibu Mkurugenzi Mkuu, muda wa ofisi yaani "*tenure",* kazi na uwezo wa kisheria wa Mkurugenzi Mkuu, Wafanyakazi na Maafisa wa Mamlaka, Kinga ya adhabu kwa maafisa, ukasimu yaani "*delegation"* kwa baadhi ya kazi za Mamlaka; na mgongano wa maslahi yaani "*conflict of interest".*

Sehemu ya Nne, inaainisha kuhusu uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi ikiwemo utekelezaji wa hatua za usimamizi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi udhibiti wa nguvu ya uvuvi, katazo la matumizi ya mitego haramu, katazo la kuvuna viumbe adimu na vyenye kutoweka, kufanya tafiti za samaki katika ukanda huo wa *EEZ*, uanzishwaji wa mipango ya uvuvi katika eneo hilo la *EEZ* na maeneo ya katika *EEZ* na uhifadhi wa mazingira ndani ya ukanda huo wa *EEZ.*

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tano, sehemu ndogo (a) imeainisha masharti ya ujumla kwa meli za uvuvi, kufuata masharti ya leseni, ruhusa na kibali cha uvuvi, sharti la kutotumika meli za uvuvi kutenda kosa, sharti la uhifadhi wa mitego kwa meli ya uvuvi isiyokuwa na leseni au ruhusa ya kuvua zuio la kutofanya uhaulishaji yaani "*transshipment"* katika *EEZ* na sharti la kuomba barua ya ruhusa au "*clearance letter"* kutoka Mamlaka kwa meli inayoomba usajili Tanzania.

Aidha, sehemu ndogo (b) imejumuisha masharti ya meli za uvuvi zenye bendera ya Tanzania na watanzania wanapofanya shughuli za uvuvi nje ya mipaka ya bahari ya Tanzania na kupatiwa motisha au "*incentives"* kwa wawekezaji wazawa.

Sehemu ndogo (c) imejumuisha masharti kwa meli za uvuvi za kigeni ikiwemo sharti la kuwa na wakala mzawa, makubaliano ya uvuvi ambayo Waziri au Mkurugenzi Mkuu anaweza kuingia masharti ya kuingia makubaliano ya mikataba ya ubia yaani "*jointventure"* au "*charter agreement"*.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Sita, imeainisha kuanzishwa kwa mfumo wa urajisi wa taarifa Mfumo huu utakuwa na taarifa au takwimu zikiwemo za samaki. Taratibu na masharti ya upatikanaji wa taarifa zilizokusanywa, usiri wa matumizi ya chumba cha ufuatiliaji wa nyenendo za meli na teknologia itakayotumika; na masharti mengine ya kiufundi, kubadilishana taarifa na kuwasilisha taarifa za uvuvi katika taasisi za kikanda za kusimamia uvuvi.

Sehemu ya Saba, Mhe. Mwenyekiti, imeeleza udhibiti wa viwango vya samaki na bidhaa zake kwa usafirishaji wa nje ya nchi na kutaja nyaraka zinazohitajika kwa uingizaji na usafirishaji wa samaki na bidhaa zake.

Sehemu ya Nane, imeweka masharti na wajibu wa ufuatiliaji, usimamizi na udhibiti kwa kutumia meli na ndege za doria na vyombo vyengine vya mawasiliano; Utekelezaji wa hatua za udhibiti wa bandari katika kupambana na uvuvi haramu. Kutangazwa kwa bandari za uvuvi na kutungwa kanuni zitazoelezea ukaguzi wa meli za uvuvi na matumizi ya bandari; na Ufuatiliaji wa meli ya uvuvi iliyofanya au kushukiwa kufanya uvuvi haramu Tanzania na kukimbia nchi jirani.

Sehemu ya Tisa, imeweka utaratibu wa kukamata, kuzuiwa au kuachiwa kwa dhamana meli ya uvuvi ya kigeni na mabaharia, kuuza, kutaifisha au kuachiwa vifaa au samaki waliokamatwa ama kuhusishwa na makosa.

Sehemu ya Kumi, imeweka masharti ya kutumika kwa Sheria ya Mamlaka kwa makosa yaliyofanyika nje ya ukanda wa eneo maalum la kiuchumi la *EEZ* ya Tanzania; na Makahakama kuu ya Tanzania Bara na Zanzibar kuwa na mamlaka ya kisheria kusikiliza makosa hayo;

Uwajibikaji wa mmiliki wa meli kwa makosa yanayofanywa na mabaharia hadi pale itakapothibitishwa vyenginevyo; na kuwajibika kwa mkosa kulipa fidia kwa hasara yoyote iliyotokana na kosa husika gharama za utunzaji wa kidhibiti na kesi.

Sehemu ya Kumi na Moja, imeeleza kuhusu ushahidi wa taarifa za doria za ndege au meli, ushahidi wa mwangalizi au mkaguzi wa uvuvi na taarifa za nyenendo za meli.

Sehemu ya Kumi na Mbili, imeeleza vyanzo vya fedha na Mamlaka; mgao wa fedha kwa SMT, SMZ na Mamlaka; makadirio ya makusanyo na matumizi ya mamlaka ya mwaka kuwasilishwa kwa Kamati Tendaji kwa kuidhinishwa; uwekezaji wa fedha za mamlaka; mafao kwa wajumbe wa kamati za mamlaka; kuwasilishwa kwa taarifa za kimahesabu za Mamlaka Bungeni na Baraza la Wawakilishi; Mkurugenzi Mkuu kutayarisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za Mamlaka; na taarifa za kifedha kila inapofika mwishoni mwa mwaka wa fedha; uwezo wa kukopa kisheria na kuanzishwa kwa bodi ya wazabuni ya mamlaka.

Sehemu ya Kumi na Tatu, imebainisha makosa na adhabu mbali mbali kama yalivyoainishwa kupitia vifungu viliyoanzisha kosa katika jadweli la pili na kujumuisha adhabu hizo; adhabu ya ujumla; kumnyang’anya mkosa faida aliyoipata kupitia kosa alilolifanya; uwezo wa Mahakama kuamrisha adhabu ya ziada na kutoa fidia; adhabu ya kurejea makosa; amri ya zuwio na kufifilisha makosa *compounding of offences*.

Sehemu ya Kumi na Nne, imeainisha uhusiano wa sheria hii na sheria nyengine, utaratibu wa utoaji wa taarifa yaani “*notification”* kwa maandishi, uwezo wa kuingia mkataba na taasisi za Tanzania Bara na Zanzibar ikiwemo kubadilishana taarifa za kisayansi; kuimarisha mashirikiano na taasisi zenye kazi zinazofanana na Mamlaka, vile vile suala zima la rufaa, kutungwa kwa kanuni lengo la kutekeleza sheria hii. Aidha, kufutwa kwa sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu na kutambulika kisheria leseni, ruhusa ya uvuvi au vibali vilivyoidhinishwa kupitia sheria iliyofutwa.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeshirikiana bega kwa bega na Wizara ya Mifugo na Uvuvi ya Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika matayarisho ya Sheria ya Kusimamaia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020. Aidha, sheria mpya imetayarishwa kwa kuzingatia maoni na ushauri uliotolewa na wadau katika vikao mbali mbali ikiwemo;

Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ), Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi (SMZ), Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Zanzibar, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (SMT na SMZ); *DSFA*; *TASAC*; *ZMA*; Bodi ya Mapato Zanzibar (*ZRB*), Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), *Nordenfjeldeske Development Services (NFDS) Africa; TAFIRI; ZAFIRI; ZAFICO; IMS; UDSM; WWF; SUZA; Agents and Associates; Bahari Foods Ltd; Zanzibar Investment Promotion (ZIPA); Tanzania Investment Centre (TIC); FETA; Tanzania Tuna Fishery National*

*Alliance (TNA); Tanzania Fisheries and Maritime Worker Union (TAFIMU); Zanzibar Seafarers Union (ZASU); ZEMA na NEMC.*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo ya jumla kuhusiana na sheria husika naomba kuorodheshwa katika Baraza la Wawakilishi Sheria ya Kusimamia na Kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu Sura ya 388 ya mwaka 2020 kwa lengo la kukidhi matakwa ya Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri, tunakushukuru kwa kuwasilisha sheria hiyo mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Waheshimiwa Wajumbe sheria hiyo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mara baada ya kumalizika kuwasilisha na Mhe. Waziri mwenye dhamana sasa inaweza kutumika kwa pande zore mbili za Muungano na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar hatutoweza kuuijadili wala kuihoji hivyo nitamke tu kwamba imepokelewa na sasa inaweza kutumika.

**Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Mwenyekiti, naomba niliombe Baraza lako tukufu kwamba hoja hii baada ya kuwasilishwa na Mhe. Waziri tupate muda kidogo baada ya kupata muda huo tutakuja kutoa msimamo wa serikali kuhusiana na hoja hii. Hivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti, tuendelee na hoja nyengine, ili utupe nafasi ya kuzingatia hoja hii kwa makini zaidi. Naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba niwahoji hoja iliyotolewa na Mhe. Waziri wanaokubaliana na hoja hiyo wanyanyue mikono, wasiokubaliana nayo, waliokubali wameshinda. *(Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Hoja ya Mhe. Waziri ya kusubiri kwa muda ili kuipa nafasi serikali kuendelea na taratibu nyengine za kisheria imekubaliwa, hivyo katibu kwa shughuli inayofuata.

## TAARIFA YA SERIKALI

### Ripoti za Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ya Mwaka 2020

**Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naanza kushukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehma kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kuwasilisha Ripoti hii ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kwa mwaka 2020 mbele ya Baraza lako tukufu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu, azidi kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kusimamia masuala ya Utawala Bora na Mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kutumia fursa hii kupiti Baraza lako tukufu kumpongeza na kumshukuru Dkt. Hussein Ali Mwinyi Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada anazofanya katika kusimamia Utawala Bora nchini kwa kuhimiza uwajibikaji, nidhamu na uzingatiaji wa sheria katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo mapambano dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukuwa fursa hii vile vile kutoa pole kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Chama cha *ACT* Wazalendo na wananchi wote kwa jumla kwa kuondokewa na Makamu wa Kwanza wa Rais, *Insha-Allah* Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho ya marehemu. Amin

Aidha, napenda kuchukuwa nafasi hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi zake mbali mbali anazochukuwa za kumsaidia Mhe. Rais katika kujenga nidhamu katika nchi yetu.

Pili, nawatakia kila la kheri wateuliwa wote katika kupambana na suala zima hili la rushwa katika jitihada za kuimarisha Utawala Bora hapa Zanzibar.

Tatu, napenda kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Mhe. Spika, Naibu Spika, na Mwenyekiti mwenza vile vile kwa jitihada mnazochukuwa kuendesha na kusimamia Baraza hili.

Aidha, naomba kuchukuwa fursa hii kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa pamoja katika jitihada wanazochukuwa katika kuchangia mambo mbali mbali yanayohusiana na maendeleo ya nchi yetu na *Insha-Allah* Mwenyezi Mungu ajaalie wachangia kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile natoa shukurani zangu za dhati kwa viongozi wote walioteuliwa na Mhe. Rais kwa kuendelea kumsaidia katika kutekeleza majukumu yao mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshukuru na kumpongeza Mhe. Hassan Khamis Hafidh Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Baraza la Wawakilishi na Mwakilishi wa Jimbo la Welezo kwa kuteuliwa na kuiongoza kamati hii Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa kamati, naahidi kwamba nitashirikiana na kamati hii na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi katika utekelezaji wa majukumua ya afisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, Majukumu ya Mamlaka ya Kuzuia Rushawa na Uhujumu Uchumi Zanzibar. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar *ZAECA* ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya kifungu namba 3 (1) cha Sheria namba 1 ya 2012 Sheria ya Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa utekelezaji wa Sera za Utawala Bora hapa Zanzibar.

Kwa mujibu wa sheria hiyo mamlaka inamajukumu ya kutoa elimu kwa jamii juu suala zima la kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, kufanya udhibiti na kubaini mianya na

matendo yote yanayoashiria kwa rushwa na uhujumu uchumi na kufanya uchunguzi kutokana na tuhuma mbali mbali zinazohusiana na uwepo wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Aidha kifungu cha 33(1)(6) cha Sheria namba moja ya mwaka 2012 kinaendelea Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na kuiwasilisha kwa waziri anaeshughulikia masuala ya rushwa na uhujumu uchumi na hatimae kuiwasilisha ripoti hii katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kuiwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Ripoti ya Jitihada ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ya mwaka 2020 kama Sheria inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, madhumuni ya Ripori hii ni kueleza Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, ili Wajumbe wa Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla waweze kuelewa vyema juhudi hizo za serikali katika kupambana na mapambano dhidi ya  rushwa na uhujumu uchumi hapa Zanzibar.

Ripoti, inaelezea kwa muhtasari hatua za utekelezaji wa udhubiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi zilizochukuliwa na serikali pamoja na kutoa mapendekezo yatakayosaidia mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii pia inahusisha taarifa ya uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi kinga na elimu kwa umma, mafanikio yaliyopatikana changamoto na matarajio.

Mhe. Mwenyekiti, Ripoti za Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ya 2020 ambayo Wajumbe wanayo nakala hiyo imegawika katika sehemu kuu tatu zifuatazo.

Sehemu ya Kwanza, ni utangulizi ambapo ipo katika ukurasa wa kwanza na inaelezea masuala mbali mbali ya rushwa ikiwemo mkataba wa Umoja wa Kimataifa, Mapambano dhidi ya Rushwa na Mkataba wa Umoja wa Kiafrika wa Kuzuia na kupambana na Rushwa.

Shemu ya Pili, ambayo imeanzia ukurasa wa pili hadi ukurasa wa kumi inaelezea jitihada mbali mbali za kupunguza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi zilizochukuliwa ikihusisha uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, utafutaji na upokeaji wa taarifa, matumizi ya huduma ya simu ya bure, uchunguzi na aina ya makosa yaliyowasilishwa katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Makosa yaliyotolewa, Hukumu na Jitihada za uokoaji na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa na uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2020 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imepokea tuhuma mia tatu na thalathini za makosa ya rushwa na uhujumu uchumi ukilinganisha na tuhuma mia mbili na thalathini zilizopokelewa katika kipindi kama kama hicho cha mwaka 2019 ambapo ni sawa na ongezeko la asilimia arubaini na tatu nukta tano. Kati ya tuhuma mia tatu na thalathini zilizopokelewa mwaka 2020 majalada hamsini na sita yamefungwa kutokana na kutojitosheleza ushahidi, majalada ishirini na tano yalitolewa ushauri wa kisheria na tuhuma kumi na saba zilihamishiwa katika taasisi nyengine.

Aidha majalada mia mbili thalathini na saba yanaendelea na uchunguzi ishirini na tano yamewasilishwa kwenye Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ambapo matatu kati ya hayo yamewasilishwa Mahakamani na majalada matano yametolewa uwamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii pia inazungumzia masuala ya kinga na elimu kwa umma, tunzo mbali mbali zilizotolewa kwa waandishi wa habari, utekelezaji wa mkakati shirikishi wa kuzuwia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar na ushiriki wa Zanzibar katika utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, inazungumzia mfanikio ya serikali yaliyopatikana katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi katika kipindi husika, changamoto na matarajio miongoni mwa mafanikio hayo ni kama haya yafuatayo.

1. Kuwepo kwa ongezeko la mali zilizorejeshwa serikalini na ambazo zilizopatikana kwa njia ya rushwa na uhujumu uchumi katika kipindi cha Januari hadi Disemba 2020. Jumla ya shilingi za Tanzania milioni 474,331,424.30 zimeokolewa kupitia makosa ya ukwepaji wa kulipa kodi, magendo na matumizi mabaya ya mali na mapato ukilinganishwa na shilingi milioni 275,717,302 zilizookolewa mwaka 2019, sawa na ongezeko la asilimia 72.03.
2. Kuwepo kwa utashi wa kisiasa katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi na kupelekea wananchi kujenga imani na kutoa ushirikiano mkubwa uliosaidia uibuaji wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo mbali mbali.
3. Kuwepo kwa mwitukio mzuri wa ofisi za umma na wananchi katika utekelezaji wa mikakati shirikishi wa kuzuwia rushwa na uhujumu uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana katika kipindi hicho, bado kuna changamoto mbali mbali ambazo zinakwamisha jitihada za serikali kukabiliana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Ikiwemo uhaba wa wataalamu wa uchunguzi wa tuhuma kubwa, ufinyu wa bajeti ya mamlaka na muundo wa taasisi.

Mhe. Mwenyekiti, matarajio ya serikali katika kukabiliana na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi ni kuendeleza jitihada ya kutoa elimu kwa umma juu ya athari ya rushwa na uhujumu uchumi, na namna ambavyo wananchi watashirikiana na serikali katika mapambano haya pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa mamlaka kwa kuwapatia mafunzo ya fani mbali mbali na vifaa vya uchunguzi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kiufanisi. Sehemu hii ipo katika ukurasa wa 11 hadi 12.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ni matumaini yangu kwamba, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu tayari wameelewa vyema jitihada za seriali katika kuzuwia rushwa na uhujumu uchumi kwa mwaka 2020, na hatua zilizochukuliwa kama nilivyoeleza katika kitabu cha ripoti ya mwaka 2020 ambacho Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wamepatiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, natoa shukrani zangu za dhati na kuipongeza Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu

Uchumi kwa kazi nzuri wanayoifanya katika mapambano dhidi ya rushwa na kuimarisha utawala bora nchini, ikiwemo matayarisho ya ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe tena kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha ripoti hii mbele ya Baraza lako tukufu, pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote kwa utulivu na usikivu wao wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri kwa uwasilishaji. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kusoma Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusu Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, muumba wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa leo hii tukiwa katika hali ya uzima na amani na kuweza kutekeleza majukumu yetu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, ninamshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kuiweka nchi yetu katika hali ya amani, utulivu, umoja na mshikamano mkubwa, hali ambayo imeendelea kuipa nafasi serikali na wananchi wake kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na mafanikio makubwa. Napenda kuwasisitiza viongozi pamoja na wananchi kwa ujumla tuendelee kudumisha kikamilifu amani na utulivu tulionao kwani bila ya amani na utulivu hakuna maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile napenda kumpongeza na kumshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa utekelezaji wake mzuri wa majukumu yake, pia kujali kwake utawala wa sheria na utawala bora katika kipindi kifupi tu tokea ashike hatamu ya kuiongoza nchi yetu.

Aidha, kamati inampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao waliyotupatia wakati wa kuipitia ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa ajili kutoa maoni ya Kamati yetu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusu uwasilishwaji wa Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar Mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na kwa kuzingatia matakwa ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba sasa kwa ruhusa yako niwataje wajumbe waliounda kamati hii kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hassan Khamis Hafidh | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Machano Othman Said | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 8. | Ndg. Haji Jecha Salum | Katibu |
| 9. | Ndg. Salma Muhsin Haji | Katibu |
| 10. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Msaidizi wa Mjumbe |

Mhe. Mwenyekiti, aidha, nachukuwa nafasi hii kuwapongeza kwa dhati kabisa viongozi na watendaji wote wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, kwa utekelezaji wa majukumu yao, licha ya changamoto mbali mbali zinazojitokeza na kukabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuhusiana na Ripoti hii ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mbele ya Baraza lako tukufu kama ifuatavyo ...

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Makamu Mwenyekiti, samahani tu kwa kukukatisha. Lakini niwaombe tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba, wakati Mhe. Makamu Mwenyekiti anaendelea kuwasilisha wale ambao watakuwa tayari kuchangia basi wawasilishe majina yao ili niweze kuyaweka kwenye orodha. Nakushukuru, endelea.

**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:** Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza sana juhudi za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, kwa kukidhi matakwa ya kifungu cha 33 cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, namba 1 ya mwaka 2012.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imefurahishwa sana na mwamko uliopatikana kwa wananchi juu ya kutoa taarifa na malalamiko yanayohusiana na viashiria vya makosa ya rushwa na uhujumu wa uchumi, ambapo ripoti hii imeonesha ongezeko la asilimia 43.5 kulinganisha na mwaka 2019. Hali hii inaonesha mafanikio makubwa ya kuweza kutokomeza kabisa rushwa na uhujumu wa uchumi nchini.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, imeanzisha juhudi za kuweka huduma ya simu ya bure, nambari 113 kwa wananchi ili kurahisisha huduma ya mawasiliano, hasa katika utoaji wa taarifa zinazohusiana na rushwa na uhujumu uchumi. Lakini kamati imesikitishwa sana kuona kuwa wapo baadhi ya wananchi hutumia vibaya fursa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza sana Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar, kwa kufanikiwa kuokoa na kurejesha serikalini mali zenye thamani ya shilingi za Kitanzania 474,631,424 zilizotokana na matumizi mabaya ya ofisi na mengineyo. Hali hii itasaidia kuondokana na uvunjifu wa sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, inapongeza hatua ya utoaji wa elimu kwa wananchi kupitia vyombo mbali mbali, ambapo inaamini kuwa hatua hii ndiyo iliyopelekea mwamko kwa wananchi kuweza kutoa taarifa na malalamiko juu ya viashiria vya kufanyika kwa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi. Hivyo, kamati inaiomba mamlaka kuhakikisha kuwa inaendelea kutoa elimu pamoja na kubuni njia nyengine ambazo wataweza kuifikia jamii yote nchini.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla kamati yetu imeridhika na Ripoti ya Jitihada za Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar ya mwaka 2020, kwa kuzingatia msingi wa kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi kilichotajwa hapo juu, pamoja na ufafanuzi uliotolewa na Mhe. Waziri na watendaji wake kutoka taasisi husika, ambapo kazi hizo zilitekelezwa kwa kuonesha ufanisi wa hali ya juu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia ripoti hii, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar imeelezea changamoto mbali mbali inazokabiliana nazo, kamati inaiomba serikali kuzifanyia kazi changamoto hizo katika kuhakikisha kuwa zinaondoka kabisa, ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii, na pia nizidi kuwashukuru wajumbe wa kamati yangu kwa mashirikiano yao makubwa waliyonipatia, pamoja na kuwa na msimamo na umakini kwa wanachokisimamia. Aidha, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kuisoma na kuifahamu vyema ripoti hii, ili tuweze kuona mambo mbali mbali yaliyoelezwa katika ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, Naomba Kuwasilisha. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa uwasilishaji wako mzuri. Waheshimiwa Wajumbe, niendelee kuwakumbusha tena sijapata bado orodha ya wachangiaji.

Waheshimiwa Wajumbe, ndio nimepokea hapa. Kwa hivyo, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum. Kwa hivyo, niendelee tena kuwahimiza kwa wale ambao wana *interest* ya kuchangia walete majina yao. Mhe. Saada karibu.

**Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum:** Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, pia namshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia taarifa hii. Lakini kipekee vile vile namshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuipa uzito taasisi hii kuweza kushughulikia vitendo hivi vya rushwa pamoja na uhujumu uchumi. Yeye mwenyewe anachukia hilo na ameona kwamba basi ni wakati sahihi wa kuweza kuipa meno na kuiwezesha zaidi taasisi yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti ki kweli na mimi nawapongeza na naunga na Mwenyekiti wa Kamati kupongeza Taasisi yetu hii ya *ZAECA* kwa kazi ambayo inaendelea kuzifanya. Huko nyuma mara nyingi *ZAECA* ilikuwepo lakini hatukuona *activeness* yake na tulikuwa tulikuwa tunasema sisi Zanzibar labda tulihisi tupo peponi, lakini *actually* hizi changamoto zilikuwepo na sasa hivi kwa kuwa *ZAECA* imepewa ndugu zaidi inafanya kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, chombo chetu hiki kimefanya jitihada kubwa na kinaendelea kufanya jitihada kubwa. Kikweli tuseme tu tufananishe labda kama taasisi nyengine, kama TAKUKURU ambayo pia yenyewe inafanyakazi kubwa. Kwa hivyo, maoni yangu *ZAECA* vile vile pamoja na mafunzo mengine ambayo ni ya *professional* ambayo wataendelea kupewa kama alivyosema Mhe. Waziri, kuna mafunzo ya kawaida. Kwa mfano, ya *customer care*, sio kila mtu anayeitwa *ZAECA* ni muhalifu, sio kila mtu anayeitwa aende *ZAECA* awe *treated un fearly.*

Nadhani hii *ZAECA* ichukuwe mifano ya taasisi kama hizi, zinapowaita watu zinakwenda kuwahoji, wawachukulie ni binadamu na kuwe na *customer care* mazungumzo yao kwa utaratibu wawaambie kama kuna usajili wafanye usajili, na hata lugha yao iwe nzuri, kwa sababu *ZAECA* inafanyakazi na watu.

Kwa hivyo, ili kupata *cooperation* zaidi *ZAECA* iteremke chini na iwe kama taasisi ambayo inatoa huduma kwa watu. Katika hili Mhe. Waziri mbali na *profession training* ambayo utawapa, vile vile tuwaambie jinsi gani waweze kuwa-*care* watu ambao wanakwenda aidha kwa kutoa taarifa au wanakwenda kwa kuhojiwa zaidi, au wanakwenda kwa kufanya mambo mengine, *customer care* haipo kwa sasa pale *ZAECA* na ushauri sasa hili lifanyike pale *ZAECA*.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili *ZAECA* vile vile inashughulikia masuala ya uhujumu uchumi na miongoni mwa hayo ni pamoja na labda wanachelewa kwa sababu moja au nyengine ya kutokulipa kodi wanazostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, *ZAECA* isiwe ndio *ultimatum*, ni lazima hizi jitihada za ulipaji kodi ziwe zinafanywa kwanza na viongozi wa taasisi husika. Kwa mfano, tuchukulie Shirika letu la Nyumba la Zanzibar utaratibu wake wa kulipa kodi ulivyo, mpaka mtu sasa anashindwa kwenda kulipa kodi anapelekwa *ZAECA*.

Kwa kweli, kinachotokea ni kwamba unakwenda kwanza pale ofisini kwao iko Shangani, unakwenda kuchukua *invoice* yako *whatever* ya malipo unachotakiwa kulipa. Ukitoka pale unakwenda zako *PBZ* ambapo ndipo kwenye *account* ya malipo. *PBZ* yetu tunaijua jinsi ilivyo, ukishakufika pale unalipia *PBZ*, ukitoka pale *PBZ* unapewa risiti yako ya malipo, unakwenda zako tena kule Shirika la Nyumba kwa ajili ya kuonesha risiti, risiti hiyo ndio unaandikiwa risiti ya kuwa umelipia. Sasa tuangalie huo mzunguko, mara nyengine kunakuwa na ugumu wa kufanya malipo kwa sababu hakuna urahisi wa kufanya malipo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe nina nyumba Dodoma nimeilipia, nakaa nyumba ya *NHC* Dodoma. Bili yako ya mwezi inakuja katika simu tu na wewe unalipia kwenye simu tu na risiti yako unatumiwe kwenye simu. Wakati mimi niko Zanzibar nafanya malipo Dodoma. Sasa utaratibu kama huu unawakwaza. Utaratibu unaofanyika huu wa Shirika letu la Nyumba. Kwa mfano unakuwa unakwaza sana *in such way* inawafanya watu wasiweze kuwa *comply on time*. Matokeo yake unachukuliwa unapelekwa *ZAECA* umehujumu uchumi. Lakini kuna jitihada gani imefanyika hapa ili kuwafanya watu waweze ku-*comply* na sheria.

Sasa hili naona Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mamlaka nyengine tuangalie. Mimi nimetoa mfano mmoja, lakini kuna mifano mingi mingine ambayo inakuwa inawakwaza watu, hususan walipa

kodi kuona kwamba kuna ugumu yaani kama kutakuwa kuna urasimu fulani. Nimemsikia Mhe. Waziri alisema wanajaribu kutayarisha utaratibu mzuri zaidi wa kielektroniki.

Lakini hapa *issue* ni kwamba *E Government* ipo na moja ya madhumuni makubwa ya *E Government* yalikuwa ni pamoja na *E Tax*, kuweka mifumo ambayo tutaweza kulipia kodi, lakini mpaka leo hii mifumo yaijakaa, lakini watu wakiwa wanapata hizo changamoto wanapelekwa *ZAECA*. *ZAECA* sio polisi, *ZAECA* sio Mahakamani, lakini vile vile *ZAECA* ijuwe kwamba kuna changamoto zinawakwaza watu ndio mpaka inafikia hiyo hatua.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba pamoja na mambo mengine tuhakikishe kwamba kuna utaratibu mzuri wa watu kuweza kwenye hili kuweza kulipa kodi, ili wasiwekwe katika kundi la wanaohujumu uchumi, taasisi hizi kwanza zenyewe zikae vizuri kabla ya kuweza kuwachukua watu na kuwapeleka *ZAECA*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nadhani mambo yangu yalikuwa hayo mawili. Nashukuru na naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nawapongeza sana *ZAECA* na waendelee kufanya kazi hii nzuri ambayo wanaifanya. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Saada Mkuya. Waheshimiwa Wajumbe majadiliano bado yanaendelea, lakini mezani kwangu sina orodha ya mchangiaji hata mmoja. Kwa hivyo, naomba sasa nimwite Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kujumuisha. Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:** Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na niwashukuru na wajumbe. Naona *ZAECA* haichangiwi sana haiulizwi sijui tuna mashaka gani, lakini hii ni kwamba wako safi, wako vizuri hawana wasi wasi na mambo yanakwenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Saada Mkuya Salum ambaye ni pekee aliyeuliza swali na kutaka ufafanuzi. Aliyoyazungumza nimeyapokea na niwajibu wa serikali kuwa sikivu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni sikivu sana katika haya. Sio busara wala sio hekma kama mtu hajalipa kodi ya nyumba ukampeleka *ZAECA* moja kwa moja. Ni kweli taasisi zipo zinazosimamia kodi kama shirika lenyewe kupitia vyombo vinavyohusika, basi wachukuwe hatua hizo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka nitanabahishe vile vile kwamba kutokulipa kodi ni kosa vile vile kwa mujibu wa sheria. Sasa kodi ndio zinasaidia kuleta maendeleo, ndio zinasababisha mambo yote Waziri wa Fedha na Mipango hapa kila wakati anatuhimiza kodi, kodi. Tukipata kodi ndio mambo yetu yanakuwa mazuri katika nchi yetu. Sasa kama anakaa katika nyumba ya serikali ni wajibu wake yeye ajue kwamba anawajibu wa kulipa kodi kwenye nyumba ile.

Serikali imegharamika imetengeneza nyumba ile na wewe umewekwa pale umekaa hulipi kodi, basi itakuwa unafanya kosa na ni makosa kwa mujibu wa sheria. Isipokuwa ni ule utaratibu wenyewe unatumika tu, yaani utaratibu wenyewe wa kwenda kuidai ile kodi yenyewe. Huwezi kwenda kumchukua mpangaji ukampeleka *ZAECA* na ukifika *ZAECA* kule kasema yeye si Mahakamani wala polisi lakini kuna taasisi ukienda unaogopa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, nilipokuwa mdogo maeneo ya Mahakamani nilikuwa sipiti wasi wasi wangu nikipita pale nitaitwa na nina ushahidi siku moja. Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako unapofika Mahakamani unaambiwa usifanye zogo usizungumze hasa kuna mtu mmoja kule shamba kwetu Makunduchi Mahakamani akawa yuko pale, zamani ilikuwa kunakuja mabasi yale mako makuu yake Kijangwani pale sasa na yeye anasafiri anataka kwenda Mjini na basi lishafika pale na yuko Mahakamani sasa atasikiaje dereva akapiga kilele pale dereva mwambie anisubiri huyo akabebwa Kizimbani akahukumiwa kama kafanya zogo Mahakamani bila kutegemea.

Kwa hivyo, ni masuala ya ambayo ya kuogopesha sana Mahakamani ni mahali pa heshima kama vile unakwenda Hospitali kwa shida kwamba unaumwa, na kwenda *ZAECA* uende kwa sababu ya kosa kubwa umelifanya. Lakini wanayo haki ya kumwita yeyote kumhoji pindipo zikipatikana taarifa. Tumeona kwenye ripoti kuna watu walituhumiwa lakini tukagundua kwamba hayana msingi mambo yale yaliyotuhumiwa na tumeyaachia na tunaendelea na hatua.

Hata hawa ambao sasa hivi tumewasimamisha serikali imechukua hatua ya kusimamisha wafanyakazi, watumishi ambao hawakutenda vizuri wametuhumiwa tunafanya uchunguzi tukibaini kwamba hawana makosa na Mhe. Rais keshasema tutawarejesha kazini na haki zao zote watazipata na yule atakae bainika katenda kosa basi hatua za kisheria zitachukuliwa.

Kwa hiyo, Mhe. Saada Mkuya Salum nikushukuru na mimi nakuahidi kwamba tutalisimamia vizuri na *Inshaa-Allah* tutakwenda vizuri, nchi yetu Zanzibar tunataka iwe hata harufu ya rushwa sio dalili hata harufu ya rushwa isikuwepo na inawezekana tukishirikiana pamoja Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe nimepokea taarifa kuwa tayari serikali imeshajiridhisha kuhusu sheria yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hivyo, nimuombe Mhe. Waziri aliyetoa hoja. Mhe. Waziri karibu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nilitoa hoja kwamba serikali ipate muda kwa sababu kulikuwa kuna mambo mawili matatu tulitaka kujiridhisha na tayari tumeshajiridhisha iko sawa sasa hoja hii ikubalike na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Waheshimiwa Wajumbe, kwa msingi huo baada ya serikali kujiridhisha na kwa mujibu wa takwa la kikatiba sasa sheria hiyo imeruhusika kutumika kwa pande zote mbili za Jamhuru ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo Waheshimiwa Wajumbe, naomba sasa baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa nichukue nafasi hii kuwahoji wanokubaliana na taarifa hiyo wanyooshe mikono na wanaokataa, basi waliokubali wameshinda. *( Makofi)*

**Mhe. Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:** Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**Mhe. Mwenyekiti:** Baada ya maelezo hayo Waheshimiwa kwa mujibu wa ratiba yetu ya leo tulitakiwa kujadili agenda tatu ambazo ni taarifa kuhusu Ripoti ya Jitihada ya Kuzuia Rushwa na Uhujumi Uchumi Zanzibar ya mwaka 2020, pili hoja ya kuanzishwa kwa Jumuiya ya Wawakilishi wanaosaidia katika mapambano zidi ya rushwa na ya tatu ilikuwa hoja ya kuanzishwa Jumuiya ya Wawakilishi kuhusiana na mabadiliko ya tabu ya nchi.

Tumemaliza ajenda ya kwanza ya taarifa ya serikali kuhusu Ripoti ya Jitihada ya Kuzuia Rushwa katika kikao hiki ilikuwa tuendelee kujadili hoja za kuanzishwa jumuiya nilizozitaja katika kikao chetu cha jioni lakini kutokana na hoja kwamba imeonekana ni busara Wajumbe kujengewa uwezo na uelewa mkubwa kuhusiana na hoja hizo kikao cha leo jioni hakitakuwepo ili kutoa nafasi kwa Wajumbe kupata uelewa wa hoja hizo nilizozitaja.

Kwa msingi huo hoja za kuanzishwa kwa jumuiya hizo mbili hazitajadiliwa na hivyo, hakutakuwa na kikao cha jioni kama nilivyotangulia kusema. Baada ya maelezo hayo sasa nachukua fursa hii kuakhirisha kikao cha Baraza hadi tarehe 24 Febuari, 2021, saa 3:00 za Asubuhi.

*(Saa 5:37 mchana Baraza liliakhirishwa mpaka*
*tarehe 24 Februari,2021 saa 3:00 asubuhi)*